# Nipashe

Jumamosi Januari 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580462

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Wamiliki** 'Day care' watakiwa kuajiri wataalamu kulea...

UKURASA 3



**Hospitali** iliyojengwa kwa fedha za Uhuru yaanza kutibu...

UKURASA 4



**Barcelona, Messi washindwa rufani**

UKURASA 20

# MATOKEO KIDATO IV

• **NECTA** yasema ufaulu umepanda kwa 5.19%, matokeo 215 yafutwa...

*Endelea ukurasa 2, 3, 5*



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Charles Msonde

## SHULE 10 BORA

1. St. Francis
2. Ilboru
3. Canossa
4. Kemebos
5. Bethel Sabs Girls
6. Feza Boy's
7. Ahmes
8. St. Aloysius Girls
9. Marian Boy's
10. St. Augustine Tagaste

## 10 BORA WASICHANA

| | |
|---|---|
| 1. Justina Gerald | (Canossa, Dar) |
| 2. Layla Atokwete | (Canossa, Dar) |
| 3. Lunargrace Celestine | (Canossa, Dar) |
| 4. Catherine Mphumuhila | (Canossa, Dar) |
| 5. Happyness Matata | (Musabe Girls, Mwanza) |
| 6. Debora Mwenda | (St. Francis, Mbeya) |
| 7. Rose Kaale | (Precious Blood, Arusha) |
| 8. Wendo Manyelezi | (Marian Girls, Pwani) |
| 9. Ellin Mungunasi | (St. Francis, Mbeya) |
| 10. Nancy Mung'anzo | (St. Francis, Mbeya) |



Paul Luziga, mwanafunzi aliyeshika nafasi ya kwanza kitaifa

## 10 BORA WAVULANA

| | |
|---|---|
| 1. Paul Luziga | (Panda Hill, Mbeya) |
| 2. Timothy Segu | (Mzumbe, Morogoro) |
| 3. Isaya Rukamya | (Feza Boy's, Dar) |
| 4. Ashrafu Ally | (Ilboru, Arusha) |
| 5. Samson Mwakabage | (Jude, Arusha) |
| 6. Derick Mushi | (Ilboru, Arusha) |
| 7. Innocent Joseph | (Mzumbe, Morogoro) |
| 8. John Maro | (Msolwa, Morogoro) |
| 9. Baraka Nyigo | (Marian Boy's, Pwani) |
| 10. John Rugemalila | (Marian Boy's, Pwani) |

## Watolewa hofu vifo vya sangara Z. Victoria

UKURASA 5

## ...Kinara kitaifa huyu hapa, atamani kuwa injinia

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO **NI CHIKWENDE MALI YA SIMBA SC** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri Ikulu Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Ufaulu kidato cha nne wapanda

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA), jana limemtangaza mwanafunzi bora kitaifa katika mtihani wa kidato cha nne mwaka 2020, Paul Luziga, kutoka Shule ya Sekondari Panda Hill ya jijini Mbeya, huku matokeo kwa ujumla yakionyesha ufaulu wa watahiniwa wa shule umeongezeka kwa asilimia 5.19 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Akitangaza matokeo hayo jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, alisema jumla ya watahiniwa wa shule 373,958 sawa na asilimia 85.84 kati ya 434,654 walioufanya mtihani huo, mwaka jana wamefaulu.

Alisema kati ya waliofaulu, wasichana ni 193,672 sawa na asilimia 85.44 na wavulana ni 180,286 sawa na asilimia 86.27.

Alisema ikilinganishwa na mwaka jana watahiniwa waliofanya mtihani huo na kufaulu walikuwa ni 340,914 sawa na asilimia 80.65.

"Katika mtihani wa mwaka 2020 ufaulu wa watahiniwa wa shule umeongezeka kwa asilimia 5.19 ikilinganishwa na mwaka 2019," alisema.

Dk. Msonde alisema katika mtihani huo jumla ya watahiniwa 490,213 walisajiliwa kufanya mtihani wakiwamo wasichana 258,323 sawa na asilimia 52.70 na wavulana 231,890 sawa na asilimia 47.30.

Alisema watahiniwa wa shule waliosajiliwa ni 448,220, waliofanya ni 437,698 sawa na asilimia 97.65 na wasichana walikuwa ni 227,695 sawa na asilimia 97.11 na wavulana 210,003 sawa na asilimia 98.25.

Alisema watahiniwa 10,522 sawa na asilimia 2.35 hawakufanya mtihani huo na wakujitegemea waliosajiliwa walikuwa ni 41, 993 na waliofanya ni 38,283 sawa na asilimia 91.17 na ambao hawakufanya walikuwa ni 3,710 sawa na asilimia 8.83.

Dk. Msonde alisema jumla ya watahiniwa 152,909 sawa na asilimia 35.10 wamepata ufaulu mzuri wa daraja la kwanza, la pili na la tatu, wakiwamo wasichana 66,899 sawa na asilimia 29.51 na wavulana ni 86,010 sawa na asilimia 41.17.

Alisema ikilinganishwa na mwaka 2019 waliopata ufaulu mzuri kwa madaraja hayo walikuwa ni 135,301 sawa na asilimia 32.01 na kwamba ubora wa ufaulu umeongezeka kwa asilimia 3.09.

Dk. Msonde alisema takwimu zinaonyesha watahiniwa wamefanya vizuri zaidi katika masomo ya msingi kwa ufaulu kuwa juu ya wastani kati ya asilimia 50.53 na 94.83.

"Watahiniwa hawakufanya vizuri katika masomo mawili Fizikia na Hesabu, japokuwa katika somo la Fizikia ufaulu umeendelea kuimarika kutoka asilimia 48.38 kwa mwaka 2019 hadi asilimia 48.87 kwa mwaka 2020," alifafanua.

**WANAFUNZI 10 BORA KITAIFA**

Paul Luziga (Panda Hill, Mbeya), Justina Gerald (Canossa Dar), Timothy Segu (Mzumbe, Morogoro), Isaya Rukamya (Feza Boy's Dar), Ashrafu Ally (Ilboru, Arusha), Samson Mwakabage (Jude Arusha), Derick Mushi (Ilboru Arusha), Layla Atokwete (Canossa Dar), Innocent Joseph (Mzumbe, Morogoro) na Lunargrace Celestine (Canossa Dar).

**WASICHANA 10 BORA KITAIFA**

Aliwataja kuwa ni Justina Gerald (Canossa, Dar), Layla Atokwete (Canossa, Dar), Lunargrace Celestine (Canossa, Dar), Catherine Mphumuhila (Canossa, Dar) na Happyness Matata (Musabe Girls, Mwanza).

Wengine ni Debora Mwenda (St. Francis, Mbeya), Rose Kaale (Precious Blood, Arusha), Wendo Manyelezi (Marian Girls, Pwani), Bellin Mungunasi (St. Francis, Mbeya na Nancy Mung'anzo (St. Francis, Mbeya).

**WAVULANA 10 BORA KITAIFA**

Dk. Msonde aliwataja kuwa ni Paul Luziga (Panda Hill, Mbeya), Timothy Segu (Mzumbe, Morogoro), Isaya Rukamya (Feza Boy's, Dar), Ashrafu Ally (Ilboru, Arusha) na Samson Mwakabage (Jude, Arusha).

Wengine ni Derick Mushi (Ilboru, Arusha), Innocent Joseph (Mzumbe, Morogoro), John Maro (Msolwa, Morogoro), Baraka Nyigo (Marian Boy's, Pwani) na John Rugemalila (Marian Boy's, Pwani).

**SHULE 10 BORA KITAIFA**

Alizitaja kuwa ni St. Francis, Ilboru, Canossa, Kemebos, Bethel Sabs Girls, Feza Boy's, Ahmes, St. Aloysius Girls, Marian Boy's na St. Augustine Tagaste.

**10 ZILIZOONGOZA MIAKA 3 MFULULIZO**

Katibu huyo alizitaja na mikoa kwenye mabano kuwa ni Santakagwa (Rukwa), Mt. Carmel (Kigoma), Trust Patrick (Arusha), Famgi (Mwanza), Kimali (Simiyu), St. Rufino and Ronaldo AGR (Kigoma), Ilboru (Arusha), Rocks Hill (Mwanza), Songea Boys (Ruvuma) na Msalato (Dodoma).

Dk. Msonde aliitaja mikoa mitatu iliyofanya vizuri zaidi kuwa ni Arusha, Kilimanjaro na Iringa na iliyoongeza ufaulu miaka mitatu mfululizo ni Lindi, Mwanza na Arusha.

Alisema halmashauri 10 zilizofanya vizuri zaidi ni Bagamoyo, Bukoba (M), Meru, Njombe (M), Bariadi (M), Kibondo, Moshi (M), Kibaha, Moshi na Mtwara (M).

Kwa upande wa halmashauri zilizoongeza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Madaba (Ruvuma), Liwale (Lindi), Moshi M (Kilimanjaro), Kibaha (Pwani), Nsimbo (Katavi), Tandahimba (Mtwara), Misungwi (Mwanza), Masasi M (Mtwara), Iringa (Iringa) na Kwimba (Mwanza).

Alisema takwimu za Mtihani wa Maarifa (QT), zinaonyesha kuwa jumla ya watahiniwa 4,446 sawa na asilimia 55.19 ya watahiniwa 8,056 waliofanya wamefaulu. Alisema kwa mwaka 2019 jumla ya watahiniwa 7,070 sawa na asilimia 62.09 walifaulu mtihani huo.

Alisema Baraza limeyazuia matokeo ya watahiniwa 235 waliopata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mtihani kwa masomo yote au idadi kubwa ya masomo.

Alisema watahiniwa wamepewa fursa ya kufanya mtihani kwa masomo ambayo hawakufanya kwa sababu ya ugonjwa, mwaka huu.

## ...Kinara kitaifa huyu hapa, atamani kuwa injinia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWANAFUNZI Paul Luziga (17), kutoka katika Shule ya Sekondari Panda Hill ya mkoani Mbeya, ambaye ameongoza kwenye matokeo ya kidato cha nne kitaifa mwaka huu yaliyotangazwa jana, amesema anatamani kuwa injinia.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu akiwa jijini Dar es Salaam anakoishi na kaka yake, alisema wakati matokeo hayo yanatangazwa alikuwa hana taarifa yoyote na alikuwa amelala.

Alisema alipigiwa simu na Mkuu wa Shule ya Panda Hill, Zephania Lusanika, akimpongeza kwa kufanya vizuri kwenye matokeo hayo na kuongoza kitaifa jambo ambalo lilimshtua na hakuamini na kudhani alikuwa kwenye ndoto.

"Nimefurahi sana japo awali nilikuwa siamini, mama naye amenipigia simu akawa analia huku akinipongeza, kwa kweli nimejisikia vizuri na naamini hii ni changamoto kubwa kwenye maisha yangu ya shule na natamani kuwa injinia," alisema Luziga.

Alisema anaamini kuwa siri ya kufanya vizuri kwenye mitihani ni kumwamini Mungu na kuwa ataendelea kumwamini na kumtumikia katika maisha yake yote.

Luziga alisema katika familia yao yeye ni mtoto wa tano na wa mwisho kuzaliwa na kwamba katika kipindi cha miaka miwili iliyopita amekuwa wakilelewa na mama yao pekee baada ya baba yao, mzee Cosmas Luziga, kufariki mwaka 2018.

Kijana huyo aliwashukuru walimu wa Shule ya Panda Hill kwa kumwezesha kufanya vizuri huku akiwashukuru wazazi wake kwa kumlipia ada miaka yote aliyosoma shuleni hapo.

Alisema awali kabla ya kujiunga na masomo ya sekondari alisoma katika Shule ya Msingi Songwe, Magereza kwa sababu baba yake kabla hajafariki alikuwa askari Magereza aliyekuwa anafanya kazi kwenye Gereza la Kilimo la Songwe.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Panda Hill, Lusanika alisema mbali na kijana huyo kufanya vizuri pia hata wenzake wote 200 aliokuwa anasoma nao wamefanya vizuri. "Tunamshukuru Mungu vijana wetu wote wamefanya vizuri, lakini kupata kijana ambaye anaongoza kitaifa ni fahari kubwa sana kwetu na nawapongeza walimu wenzangu kwa kazi kubwa waliyoifanya," alisema Lusanika.

Alisema wataendelea kuhamasishana kufanya kazi kwa bidii na kuwahamasisha wanafunzi kusoma ili shule hiyo iendelee kuwa bora kitaaluma.



Wanafunzi wa shule ya Feza, wakifurahia baada ya Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), kutangaza matokeo ya mtihani wa kidato cha nne, jijini Dar es Salaam jana, ambapo shule hiyo imeingia 10 bora kitaifa na mwanafunzi wake, Isaya Rukamya kuwa mwanafunzi bora namba nne kitaifa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# NECTA yafuta matokeo 215 kwa udanganyifu

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA), limetangaza matokeo ya upimaji wa darasa la nne, kidato cha pili na mitihani ya kidato cha nne, huku vitendo vya udanganyifu vikiendelea na kusababisha waliofutiwa matokeo kufikia 215.

Kati ya watahiniwa waliofutiwa matokeo yao baada ya kufanya udanganyifu, 75 ni wa kidato cha nne, 63 ni wa upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili na 77 ni waliofanya mtihani wa upimaji wa darasa la nne.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, aliwaambia waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuwa, kabla ya kufanyika mitihani hiyo walitoa onyo kwa baadhi ya shule baada ya kupata taarifa zinajipanga kufanya udanganyifu.

Dk. Msonde alisema NECTA ilitoa onyo kwa shule 71 za sekondari baada ya kupata taarifa za kupanga kufanya udanganyifu katika mtihani wa kidato cha nne na baadaye ziliongezeka 26 zilizokuwa katika harakati hizo.

Alisema udhibiti uliofanywa maeneo mbalimbali ambako mtihani huo ulikuwa unafanyika, umesaidia kupunguza kiwango cha udanganyifu.

"Udanganyifu umepungua tunawashukuru wananchi wamesaidia kutupa taarifa za awali ambazo tulizibaini hizi shule 71 na baadaye shule nyingine 26 nazo zilitajwa.

Tunazipongeza kamati za halmashauri na mikoa kwa usimamizi mzuri, pia tunazipongeza shule ambazo zimeacha udanganyifu, tunaamini mwanafunzi hawezi kufanya udanganyifu bila ushiriki wa walimu, mwaka 2021 tuseme udanganyifu basi na tutambue ufaulu unawezekana bila udanganyifu," Dk. Msonde alisema.

Katika matokeo ya darasa la saba ambayo yalitangazwa mwezi Novemba mwaka jana, matukio ya udanganyifu yalijitokeza na mwalimu wa taaluma alidaiwa kukutwa chooni akigawa majibu kwa wanafunzi.

Katika matokeo hayo ya darasa la saba, Dk. Msonde alisema walibaini udanganyifu huo ulifanywa na wakuu wa shule 38 na kusababisha matokeo ya wanafunzi 1,059 kufutwa.

# Vyuo kutafiti janga corona lilivyoathiri upatikanaji chakula

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO Kikuu cha Ardhi (ARU), Mtandao wa Wakulima wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAFF), kwa kushirikiana na Chuo cha Westerncamp cha nchini Afrika Kusini, wapo katika utafiti wa janga la corona lilivyoathiri mifumo ya upatikanaji wa chakula barani Afrika.

Mratibu wa ESAFF Kanda ya nchi za Afrika Mashariki na Kusini, Joseph Mzinga, alisema jana kuwa utafiti huo ulianza mwezi Septemba, mwaka jana na utafanyika kwa mwaka mmoja katika nchi tatu ambazo ni Afrika Kusini, Ghana na Tanzania.

Alisema utafiti huo unaofadhiliwa na Kituo cha Kimataifa cha Maendeleo ya Utafiti (IDRC), lengo lake ni kuja na matokeo ambayo watawafahamisha watunga sera katika ngazi ya taifa na kanda ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), kuhusu kujenga mfumo imara wa upatikanaji wa chakula magonjwa kama corona yanapotokea yasilete athari.

Alisema pamoja na kuwapo kwa matatizo ya upatikanaji wa chakula kwa nchi nyingine za Afrika, Tanzania ilikuwa nacho hadi kufika hatua ya kukiuza kwa nchi nyingine.

"Mbali na corona utafiti huu utasaidia mapambano dhidi ya utapiamlo na udumavu ambapo kuna mamilioni ya watoto Afrika wanasumbuliwa na tatizo hilo, kwa upande wa Tanzania udumavu upo kwa asilimia 30," alisema.

Pia, Mzinga alisema mwezi Oktoba, mwaka huu mkutano mkubwa wa Umoja wa Mataifa (UN), unatarajia kufanyika kuhusu mfumo wa chakula katika nchi za Afrika, utafiti huo utatumika kama moja ya taarifa namna nchi inavyokabiliana na hali hiyo.

Alisema kwa Tanzania utafiti huo utafanyika katika mikoa sita ambayo aliitaja kuwa ni Mwanza, Dar es Salaam, Arusha, Kahama, Dodoma na Mbeya ambako watatembelea masoko makubwa ya chakula katika mikoa hiyo kuangalia mazao ya nafaka, matunda, samaki na nyama.

Mfanyabiashara soko la Mabibo, Enock Kimwayeya, anayeuza viazi na vitunguu, alisema corona ilipoingia nchini mwezi Aprili hadi Juni, mwaka jana, mauzo yalishuka kutokana na baadhi ya watu kuhofia kwenda mwenye msongamano.

Alisema hali hiyo ilisababisha bei ya viazi kushuka kutoka Sh. 50,000 kwa gunia hadi kufikia Sh. 25,000.

# 'Day care' zatakiwa kuajiri wataalamu malezi

**Na Mwandishi Wetu**

WAMILIKI wa vituo vya malezi kwa watoto (Day Care Centre), wametakiwa kuwa na wataalamu wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ili kutoa malezi sahihi kwa watoto wanaowahudumia katika vituo vyao.

Agizo hilo limetolewa na Dk. John Jingu, wakati akiwatunuku stashahada na astashahada wanafunzi 156 wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kisangara, mkoani Kilimanjaro.

Alisema hakuna taifa ambalo litaendelea vizuri kama msingi wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto hautochukuliwa kwa umuhimu unaostahili.

Vile vile, alisema kwa kipindi hiki jamii imekuwa ikishirikiana na serikali katika kuanzishwa na kujenga vituo vya malezi na makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika ngazi ya jamii vitakavyosaidia kulea watoto katika maeneo husika.

Alisisitiza kuwa mafunzo hayo yanayotolewa na Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama Kampasi ya Kisangara, yamekuwa ni msingi hasa katika ustawi wa watoto na familia nchini.

"Sasa ili suala hili lifanikiwe tufanye haraka kumaliza mitaala ya mafunzo ya elimu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ili mafunzo haya yaendelee kutolewa kwa vile kuna uhitaji mkubwa wa masomo haya," alisema.

Dk. Jingu aliagiza Menejimenti ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii kuendelea na uwekezaji kwenye rasilimali watu katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kisangara ili iwe mahiri kwa utoaji wa mafunzo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto nchini.

Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dk. Joyce Nyoni, aliishukuru serikali kwa kuendelea kusimamia Taasisi hiyo kwa kutoa miongozo na maelekezo yenye lengo la kuhakikisha fani ya Ustawi wa Jamii inaleta matokeo chanya katika jamii.

Mkurugenzi wa Idara ya Mashirika yasiyo ya kiserikali, Vickness Mayao, akizungumza kwa niaba ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Naftali Ng'ondi, alisema Idara ya Ustawi wa Jamii itaendelea kusimamia Taasisi hiyo ili iweze kutoa mafunzo yatakayosaidia jamii kubadilika na kuendelea.

Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara kilianza Mwaka 1986 kwa kutoa mafunzo ya Elimu ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto na mwaka 2020 kilikabidhiwa rasmi katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama.

# Wapewa siku 90 kusimamia uzalishaji ngozi

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, ametoa miezi mitatu kwa Makatibu Tawala wa mikoa kusimamia uzalishaji wa ngozi bora inayofaa kutumika katika uzalishaji wa bidhaa za malighafi hiyo viwanda vya nchini.

Aliwataka makatibu tawala hao kusimamia wakurugenzi katika halmashauri zote nchini, mnyororo wa thamani wa zao la ngozi ili lilete tija katika uchumi wa nchi.

Alisema pamoja na Tanzania kuwa na idadi kubwa ya mifugo, bado zao la ngozi halifanyi vizuri.

Prof. Gabriel alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam wakati akifunga mafunzo kwa maofisa wa sekta ya mifugo.

Alisema tatizo la uzalishaji mbovu wa zao la ngozi, linachangia kwa kiwango kikubwa kurudisha nyuma viwanda vinavyotegemea zao hilo katika uzalishaji wa bidhaa za ngozi nchini.

"Nchi yetu ni ya pili kwa wingi wa mifugo katika Bara la Afrika, lakini pamoja na mafanikio hayo, zao la ngozi bado halifanyi vizuri, kujikwaa siyo kuanguka, tujipange upya kufufua sekta hii, tunahitaji kuongeza thamani stahiki katika mazao ya mifugo ambayo ni nyama, maziwa na ngozi," alisema Prof. Gabriel.

Kadhalika, alisema kwa takwimu za kufikia juzi, Tanzania ina ng`ombe milioni 33.4, mbuzi milioni 21.29, kondoo milioni 5.6 na nguruwe milioni mbili.

"Hii ni sekta inayokua kwa zaidi ya asilimia tano kwa mwaka na inachangia kwenye pato la taifa zaidi ya asilimia saba, kwa hiyo tunatakiwa kuhakikisha tunasimamia ng`ombe kuanzia kwa wachunaji kwa sababu ukishakosea kuanzia hapo ndio unaharibu ngozi, na namna inavyohifadhiwa ili hata wanaozinunua wapate faida," alisema Prof. Gabriel.

"Ombi langu ni kwamba tumedhamiria kuboresha sekta ya ngozi kwa kasi kubwa, tunatakiwa tupambane."

Alizitaka halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba asilimia 15 ya mapato yanayopatikana katika sekta hiyo inatumika katika kuhudumia sekta hiyo.

"Na kwa kutekeleza hilo na kulisimamia kwa ufanisi naamini itasaidia kumaliza matatizo yote yaliyopo katika sekta hii ikiwamo masuala ya ngozi, matibabu, dawa na majosho," alisema Prof. Gabriel.

"Ubora wa ngozi unashabihiana na afya ya mnyama, kwa muktadha huo tunahitaji kuwekeza pia katika chanjo, unyonyeshaji na malisho na ni wakati muafaka kanuni ya uogeshaji na ya chanjo nayo isimamiwe ipasavyo."

Kwa upande wake mtaalamu wa sekta ya ngozi, Emmanuel Muyingi, alisema tatizo kubwa linalochangia uzalishaji mbovu wa zao hilo ni uchunwaji mbovu wa ng`ombe kwenye machinjio, uandaaji na uhifadhi mbaya baada ya kuchinja.

Sababu nyingine alisema ni baadhi ya machinjio kuwatumia wachunaji wasio na taaluma hiyo.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (kushoto), akimsikiliza Mkurugenzi wa Kampuni ya Madini ya Tanzanite ya Franone Mining and Gems Ltd, Onesmo Mbise (wa pili kulia), alipotembelea mgodi huo katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. Wa (pili kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Simon Msanjila. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ndugulile azibana taasisi, azipa siku 100 kujipima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amewabana watendaji wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kuandaa mikataba ya kupima utendaji kazi na kuwataka kuona mafanikio yanayopimika ndani ya siku 100.

Pia ameliagiza Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuweka mikakati ya kujiendesha kibiashara ili kukidhi soko la ushindani.

Dk. Ndugulile alitoa agizo hilo jana jijini hapa katika kikao kazi cha kujadili utendaji wa TTCL kilichowakutanisha watendaji wa shirika hilo.

Alisema ndani ya siku 100 anataka kuona mambo makubwa yakifanywa ndani ya taasisi za wizara yake ili kukidhi matarajio ya Watanzania.

"Hakuna kulala hizi siku 100, zikifika tu siku 90 tunataka matokeo yanayopimika na mtendaji wa kila taasisi atakuja mbele yangu kueleza ndani ya kipindi hicho imefanya nini, kinachopimika sio michakato," alisema.

Alisema katika mikataba hiyo atakayoingia na watendaji hao, nao watapaswa kuingia na waliochini yao ili kuwa na utendaji kazi wenye tija kwa taifa.

"Inawezekana siku za nyuma hamkuwa na mikataba, Kindamba (Mkurugenzi wa TTCL), utakuwa na mkataba na mimi wa performance (utendaji), utakuja kuniambia nini unakusudia kufanya, nikikubana wewe na wewe utaenda kubanana na wenzako," alisema. Kuhusu Shirika la TTCL, Waziri Ndugulile alisema linapaswa kujiendesha kibiashara na kuondoa vikwazo kwenye utoaji huduma kwa wananchi.

"Kumekuwapo na malalamiko kwa wananchi kama suala la upatikanaji wa vocha baadhi ya mikoa, vocha hazipatikaniki shida ipo wapi? Pia angalieni vifurushi vyenu, nyie mna advantage (faida) kuliko kampuni nyingine boresheni vifurushi vyenu, kitengo cha huduma kwa wateja pia kiboreshwe," alisema.

Aliwataka wakuu wa vitengo viwili vya masoko na utafiti wa shirika hilo kuhakikisha hawafanyi biashara kwa mazoea na badala yake wawe wabunifu.

"Mje na mikakati ambayo ni mizuri tunajua mna mahitaji ya fedha, lakini mje na mikakati inayopimika ili hata nikikupa Sh. milioni 100 basi baada ya muda uniletee Sh. milioni 300, lengo la wizara ni kuona TTCL isimame sio kwa kubebwa bebwa kuweni na ubunifu," alisema.

Kuhusu matumizi, Dk. Ndugulile alisema hayalingani na wanachokipata na kuwataka kuboresha huduma kwa wateja.

"Masuala ya fedha mtandao ni makubwa sana ndani ya nchi hivi tunavyoongea kwa mwezi tuna miamala isiyozidi Sh. milioni 300, hivyo tuna miamala Sh. milioni 100 kwa siku na kiasi cha fedha kinachozunguka kwenye miamala kwa mwezi ni takribani Sh. trilioni moja, kwa mwaka ni Sh. trilioni 12," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba, alisema kwa miaka mitano kabla ya mwaka wa fedha 2016/17 shirika hilo lilikuwa likijiendesha kwa hasara ya Sh. bilioni 15 kwa mwaka, tangu kuingia serikali ya awamu ya tano madarakani linajiendesha kwa faida ya Shilingi bilioni tano kwa mwaka.

Alisema shirika hilo lipo mbioni kukamilisha mikataba miwili mikubwa ya utoaji huduma nchini Dubai na Malawi.

"Tunatarajia ndani ya siku 90 kufunga mkataba na kampuni kutoka Dubai wa Dola za Marekani zaidi ya milioni 3.6 tatu, pia mkataba mwingine Malawi wa Dola za Marekani milioni 3.2, tunataka kufanya ubunifu ndani ya muda uliotupa," alisema.

# Hospitali iliyojengwa kwa fedha za sherehe ya Uhuru yaanza kutibu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Uhuru iliyopo Chamwino, mkoani Dodoma imeanza kutoa huduma kwa wagonjwa 300 ndani ya siku 22.

Ujenzi wa hospitali hiyo umegharimu Sh. bilioni 3.99, ambazo zimetokana na kuahirishwa maadhimisho ya Siku ya Uhuru, mwaka 2018 na gawio la kampuni ya Airtel kwa mwaka huo.

Akizungumza jana wakati akikagua utoaji wa huduma kwenye hospitali hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, aliagiza wataalamu wa afya kutoa huduma bora kwa wagonjwa.

"Nimeridhishwa na hatua iliyofikiwa, ninachotaka kuwaelezea hakikisheni mnatoa huduma bora kwa wagonjwa, pia Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Best Magoma, hakikisheni mnaendesha programu ya hospitali tembezi katika hospitali ili wananchi wengi wapate huduma za kibingwa," aliagiza.

Alisema hatua hiyo itachagiza maono ya Rais John Magufuli ya umuhimu wa hospitali hiyo, huku akimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chamwino, Athuman Masasi, kufanya kampeni ya kuhamasisha wananchi kujiunga na mfuko CHF iliyoboreshwa.

"Tunataka wananchi wetu wanufaike na matunda ya huduma za afya katika hospitali, pia watumishi hakikisheni fomu za bima zinajazwa vizuri ili kurejeshewa madai kwa haraka," alisema. Awali Mganga Mkuu, Dk. Magoma, alisema hospitali hiyo ilianza kutoa huduma za awali Desemba 21, mwaka jana kwa kuhudumia wagonjwa wa nje.

Alisema hospitali hiyo ina watumishi 53 ambao ni wa kada za afya na saidizi kutoka Chamwino, Bahi, Mpwapwa na Jiji la Dodoma.

"Pia tumefanya kampeni ya ukusanyaji damu, ambapo tumepata uniti 40 ambazo kutokana na miundombinu kutokamilika, tumeenda hifadhi Hospitali ya Chamwino na Hospitali ya Mkoa wa Dodoma," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema hospitali hiyo imeanza kutoa huduma huku baadhi ya maeneo yakiendelea na ujenzi.

Mmoja wa wagonjwa waliofika hospitalini hapo, Olivia Mchete, alisema.

"Tunashukuru sana rais wetu mpendwa Magufuli kwa kutuletea mradi huu, nilikuja Jumatatu na leo nimerudi tena kwa vipimo zaidi, hakika hospitali hii ni mkombozi kwetu, maana kimbilio kwetu lilikuwa zahanati."

# 11 washtakiwa kuendesha kilimo pori tengefu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi, Mkoa wa Morogoro imewapandisha kizimbani washtakiwa 11 kwa makosa manne tofauti likiwamo la kuendesha shughuli za kilimo cha mpunga ndani ya pori tengefu la Kilombero, mkoani hapa.

Wakisoma mashtaka yanayowakabili washtakiwa hao mbele ya Hakimu Elia Mrema, Mawakili wa Serikali waandamizi kutoka ofisi ya DPP, Theophil Mutakyawa, Salimu Msemwa, Edgar Bantulaki na Grace Mpatili, walidai mahakamani hapo kuwa washtakiwa hao wote kwa pamoja kati ya mwezi Januari, 2006 hadi Desemba, 2020, walifanya matukio mbalimbali kinyume na sheria za hifadhi.

Mawakili hao waliyataja mashtaka waliyokabiliwa nayo washtakiwa kuwa ni kuongoza mtandao wa uhalifu wa kupangwa na kuendesha shughuli za kilimo cha mpunga ndani ya pori tengefu la Kilombero, kinyume cha Sheria za Wanyamapori namba 5, 20 (1) (c) (4) ya mwaka 2009.

Waliyataja makosa mengine kuwa ni pamoja na kujihusisha na rushwa na utakatishaji fedha haramu.

Waliwataja washtakiwa wanaokabiliwa na mashtaka hayo kuwa ni pamoja na Elisante Oktavian, Vicent Mkuki, Joshua Keraryo, Samwel Tango, Pasco Peter, Bosco Jackob, Ernest Heguye, Fredrick Mujoge, Devotha Ngonyani, Mkasiwa Shabani ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Ipugasa, wilayani Mlimba na Paulo Mwambope.

Mawakili hao wa serikali walidai mahakamani hapo kuwa washtakiwa hao wote kwa pamoja huku wakijua kufanya hivyo ni makossa, walipokea na kutoa rushwa na kisha kulima na kupata mazao ambayo baada ya kuyavuna na kuuza walipata fedha na kuzitakatisha kwa kununua matrekta kwa ajili ya kuendelea na shughuli za kilimo kwenye maeneo ya pori tengefu bila kujali kuwa maeneo hayo ni ya hifadhi.

Hakimu wa mahakama hiyo, Elia Mrema, alisema, makosa ya washtakiwa hao yote hayana dhamana na kuamuru warudishwe rumande hadi Januari 18, kesi yao itakapotajwa tena huku upelelezi wa kesi hiyo ukiwa bado haujakamilika.

# 123,864, Darasa la Nne hawakufanya mtihani upimaji

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI 123,864 sawa na asilimia 6.77 kati ya 1,704,404 waliosajiliwa kufanya mtihani wa upimaji wa Darasa la Nne mwaka 2020, hawajafanya.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Charles Msonde (pichani), aliwaambia waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuwa, kati ya wanafunzi hao ambao hawajafanya mtihani huo, wasichana ni 50,599 sawa na asilimia 5.51 na wavulana ni 73,265 sawa na asilimia 8.05.



Alisema takwimu za matokeo zinaonyesha jumla ya wanafunzi 1,551,599 kati ya 1,704,286 wenye matokeo ya upimaji wameweza kupata alama zenye madaraja ya ufaulu wa A, B, C na ikilinganishwa na wanafunzi 1,531,120 waliopata madaraja hayo mwaka 2019.

Alisema kumekuwa na ongezeko la wanafunzi 20,479 sawa na asilimia 1.34 waliopata fursa ya kuendelea na Darasa la Tano ikilinganishwa na mwaka 2019.

Alisema takwimu zinaonyesha wanafunzi wamefanya vizuri kwa masomo yote na ufaulu wa chini ni asilimia 70.85 somo la Hesabu na ufaulu wa juu ni 95.46 somo la Uraia na Maadili.

**WANAFUNZI 10 BORA KITAIFA**

Jovinia Kamunyila (Peaceland, Mwanza), Abdulaziz Marwa (Peaceland, Mwanza), Charles Shilugala (Peaceland, Mwanza), Maryfaith Minja (Imani, Kilimanjaro), Baraka Mwita (Graiyaki, Mara), Beatrice Luvunda (Graiyaki, Mara), Lucy Mwita (Graiyaki, Mara) Stella Mshana (Shekina, Kilimanjaro), Wenseslaus Shayo (Imani, Kilimanjaro) na Vailet Msuya (Shekina, Kilimanjaro).

**WASICHANA 10 BORA KITAIFA**

Jovinia Kamunyila (Peaceland, Mwanza), Maryfaith Minja (Imani, Kilimanjaro), Beatrice Luvunda (Graiyaki, Mara), Lucy Mwita (Graiyaki, Mara), Stella Mshana (Shekina, Kilimanjaro), Vailet Msuya (Shekina, Kilimanjaro), Esther Mabula (Twibhoki, Mara), Naomi Joctone (Twibhoki, Mara), Noelitha Lusekelo (Twibhoki, Mara) na Joyce Masunga (Peaceland, Mwanza).

**WAVULANA 10 BORA KITAIFA**

Abdulaziz Marwa (Peaceland Mwanza), Charles Shilugala (Peaceland, Mwanza), Baraka Mwita (Graiyaki Mara), Wenseslaus Shayo (Imani, Kilimanjaro), Devis Naftary (Kemebos, Kagera), Francisco Kimila (Kemebos, Kagera), Kanisusi Malawa (Tabasamu, Mwanza), Daud Elias (Mzigu, Mwanza), Samson Shayo (Musabe, Mwanza) na Nicolaus Onessmo (Exodus, Mwanza).

**10 ZILIZOSHUKA UFAULU MIAKA 3 MFULULIZO**

Alizitaja kuwa ni Rugongwe (Kibondo), Mboghoi (Lushoto), Nkukai (Lushoto), Kalusiru (Lushoto), Kwemshwa (Lushoto), Mambo (Lushoto), Kamlale (Geita vijijini), Nyihanga (Bunda Mji), Bugaga (Kasulu) na Mtindili (Lushoto).

Alisema mikoa iliyofanya vizuri zaidi ni Dar es Salaam, Lindi na Arusha na iliyoongeza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Lindi, Dodoma na Dar es Salaam.

Halmashauri zilizoongeza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Meatu, Musoma, Songwe, Butiama, Tarime, Liwale, Igunga, Chamwino, Ruangwa na Kilwa.

Kwa upande wa upimaji wa kidato cha pili, Dk. Msonde alisema jumla ya watahiniwa 646,200 walisajiliwa kufanya mtihani huo na kati yao wasichana ni 344,339 sawa na asilimia 53.29 na wavulana ni 301,861 sawa na asilimia 46.71.

Alisema kati ya waliosajiliwa waliofanya mtihani huo ni 601,948 wakiwamo wasichana 323,987 sawa na asilimia 94.09 na wavulana 277,961 sawa na asilimia 92.08.

Alisema wanafunzi 44.252 sawa na asilimia 6.85 hawakufanya mtihani huo na kati yao wasichana ni 20,352 sawa na asilimia 5.91 na wavulana ni 23,900 sawa na asilimia 7.92.

**WANAFUNZI 10 BORA KITAIFA**

Nankondo Mnyone (Feza Girls, Dar), Tiffany Kazael (Canossa, Dar), Daraja Ahmed (Canossa, Dar), Edward Rugaimukamu (Canossa, Dar), Lukas Lutengano (Kibasila, Dar), Benjamin Mwakapalila (Feza Boy's, Dar), Namara Lwansa (Feza girls), Nuran Majid (Feza Girls, Dar), Junior Mkeni (Jude, Arusha) na Hope Semsela (Feza Girls, Dar).

**WASICHANA 10 BORA KITAIFA**

Nankondo Mnyone (Feza Girls), Tiffany Kazael (Canossa, Dar), Daraja Ahmed (Canossa, Dar), Edward Rugaimukamu (Canossa, Dar), Namara Lwansa (Feza Girls, Dar), Nuran Majid (Feza Girls Dar), Hope-Rosemary Semsela (Feza Girls, Dar), Vivian Mwantengule (Feza Girls, Dar), Rahma Ikungu (Feza Girls, Dar) na Asia Siwale (Kilakala, Morogoro).

**WAVULANA 10 BORA KITAIFA**

Lucas Lutengano (Kibasila Dar), Benjamin Mwakapalila (Feza Boy's Dar), Junior Mkeni (Jude Arusha), Collins Mkama (Feza Boy's, Dar), Albert Mtambo (Feza Boy's, Dar), Emily Ntandu (Jude, Arusha), Emmanuel Maiga (St. Anthony's, Dar), Jabber Mohamed (Imperial, Pwani), Vasco Mwambila (Chang'ombe, Dar) na Yusuph Philipo (Chang'ombe Dar).

**SHULE 10 BORA KITAIFA**

St. Francis (Mbeya), Kemebos (Kagera), Bright Future Girl's (Dar), Canossa (Dar), Tengeru, (Arusha), Centennial Christian, (Pwani), St. Monica Moshono Girls (Arusha), Marian Boy's (Pwani), Precious Blood (Arusha) na Feza Boy's (Dar).

**ZILIZOONGOZA UFAULU MIAKA 3 MFULULIZO**

Mtoni Moro (Morogoro), Oldonyosambu (Arusha), Arusha Day (Arusha), Kibasila (Dar), Cerket (Morogoro), St. Bakanja (Kigoma), Lamadi (Simiyu), St. Clara (Dodoma), Dk. Mezger (Morogoro) na St. Anselm (Iringa).

**ZILIZOSHUKA UFAULU MIAKA 3 MFULULIZO**

Ugombolwa (Dar), Manga Mpakani (Tanga), Rev.A. Bungwa (Kigoma), Msolwa (Morogoro), Kunduchi Girls Islamic (Dar), Mahaha (Simiyu), Kirua (Kilimanjaro), St. Theresa of Avila girls (Shinyanga), Ilowola (Njombe) na Mivumoni Islamic (Dar).

Dk. Msonde alitaja mikoa mitatu iliyofanya vizuri zaidi ni Arusha, Iringa na Kilimanjaro na mkoa mmoja ulioongeza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Lindi na hakuna iliyoshuka ufaulu.

# Wananchi waondolewa hofu vifo sangara

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANANCHI wameondolewa hofu ya vifo vya samaki aina ya sangara katika Ziwa Victoria na kutakiwa kuendelea na shughuli zao ili kukuza vipato na uchumi wa nchi.

Katibu Mkuu Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, kuwa mwanzoni wa mwaka huu walitokea taarifa ya vifo vya samaki aina ya sangara katika Ziwa Victoria nchini Uganda, maeneo ya Kaskazini Magharibi nchini humo.

Alisema baada ya utafiti wamebainika kuwa upande wa Tanzania vifo hivyo havijaripotiwa sehemu yoyote isipokuwa kwa wavuvi na wananchi wa eneo la Masonga-Sota, mkoani Tarime, waliodai kuona vifo vya samaki, Januari 2, mwaka huu.

"Baada ya kupata taarifa hizo Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikishirikiana na Taasisi yake ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), kituo cha Mwanza iliwasiliana na maofisa uvuvi, wavuvi na wadau wengine wa uvuvi katika Ziwa Victoria ikiwamo Chama cha Wavuvi (TAFU) na tulibaini hakukuwa na taarifa za vifo," alisema Tamatamah.

Kadhalika, alisema katika kufuatilia suala hilo waliwasiliana na Idara ya Uvuvi ya Uganda ambao walitoa taarifa ya kupeleka sampuli za samaki waliokufa katika maabara mbalimbali nchini mwao ili kujua kama kuna maambukizi ya sumu ya aina yoyote inayosababisha vifo vya samaki hao.

"Idara hiyo imeweza kutuhakikishia kuwa samaki hawakuwa na sumu na inadhaniwa kuwa vifo hivyo vimetokana na tukio la kila mwaka linalotokana na mchanganyiko wa maji ziwani kati ya tabaka la chini lenye hewa ndogo ya oksijeni na lile tabaka la juu," alisema.

Akielezea hali ya ziwa hilo katika mzunguko wa majira ya mwaka, alisema husababisha matukio mawili ambayo ni utengenezaji wa matabaka ya maji kati ya tabaka la chini lenye hewa ndogo ya oksijeni na lile tabaka la juu lenye hewa ya oksijeni ya kutosha linatokea kuanzia Januari hadi Aprili na kipindi cha mvua kubwa lingine ni mchanganyiko wa maji kati ya tabaka la juu na chini ambalo hutokea wakati wa kiangazi na upepo mkubwa kuanzia Juni hadi Septemba.

Alisema katika hali ya kawaida sangara huishi katika maji ya tabaka la kati na juu kuanzia mita 15 hadi 20 ambalo lina hewa ya kutosha ya oksijeni zaidi ya miligramu tatu kwa lita.

Vile vile, alisema wakati wa kipindi cha mchanganyiko wa maji kutoka tabaka la chini lenye hewa ndogo ya oksijeni, hupunguza kiwango cha hewa hiyo chini ya miligramu tatu kwa lita katika tabaka la kati na juu wanakoishi sangara na chini ya kiwango hicho cha hewa samaki hao hasa wakubwa hushindwa kuvumilia na kufa, hali hiyo hutokea kila mwaka au kila baada ya miaka michache.

"Pamoja na kuwa vifo hivyo havijaonekana kwenye maji ya upande wa Tanzania, kuna uwezekano kuwa mchanganyiko wa maji unaweza kutokea kwetu pia kama hali ya hewa itaruhusu wakati wa mvua kubwa na upepo mkubwa, hivyo wizara na wadau wa sekta ya uvuvi wanaendelea kufuatilia uwezekano wa kujitokeza vifo hivyo," alisema.

Alisema vitakapojitokeza, hatua za haraka zitachukuliwa ili kubaini kama vinasababishwa na chanzo kilichozoeleka cha mabadiliko ya hali ya ziwa au vinatokana na shughuli za kibinadamu ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa mapema.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dua njema kwa Stars katika fainali za CHAN

**FAINALI** za mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinatarajiwa kufanyika kuanzia leo hadi Februari 7, mwaka huu nchini Cameroon.

Michuano hiyo inafanyika chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), na moja ya malengo yake ni kuwapa nafasi wachezaji wanaoshiriki katika ligi za ndani kuonyesha vipaji vyao baada ya kukosa fursa hiyo kwenye fainali nyingine maarufu AFCON.

Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), ambayo kwa sasa inafundishwa na Kocha Mkuu Mrundi Etienne Ndayiragije ni moja ya nchi zilizokata tiketi ya kushiriki fainali hizo za mwaka huu na imepangwa Kundi D pamoja na Zambia, Namibia na Guinea.

Hii ni mara ya pili kwa Taifa Stars kupata tiketi ya kucheza fainali hizo, mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2008, tena michuano hiyo ikifanyika kwa mara ya kwanza na iliongozwa na Mbrazil Marcio Maximo, hata hivyo iliishia hatua ya makundi.

Taifa Stars itaanza kuwania ubingwa huo kwa kuwavaa Zambia maarufu Chipolopolo hapo Jumane halafu itashuka dimbani tena Januari 23, mwaka huu kucheza dhidi ya Nambia na itamaliza mechi zake za hatua ya makundi kwa kuwavaa Guinea baada ya siku nne.

Tayari kikosi cha Taifa Stars ambacho kituo chake kitakuwa kwenye Mji wa Limbe kilishawasili Cameroon tayari kuendelea na maandalizi ya fainali hizo, ikiwa ni mara yake ya pili kufuzu michuano hiyo.

Kwa sababu sisi ni Watanzania, huu ni wakati sahihi wa kuungana kuiombea dua njema Taifa Stars ili ifanye vyema katika fainali hizo na kuiletea nchi heshima ambayo inaihitaji.

Kama wadau wa michezo, tunafahamu hakuna mashindano mepesi, hakuna taifa dogo, hakuna timu ndogo, hivyo tunawaomba wachezaji na benchi la ufundi kuingia uwanjani wakiwa na nguvu na wakiamini hakuna kisichowezekana.

Maandalizi ambayo kikosi hicho kimefanya ni ishara nzuri kuwa wataingia katika mashindano hayo kupambana na si kushiriki kama ilivyozoeleka kwa miaka ya nyuma.

Wachezaji wa Taifa Stars, huu ni wakati wenu wa kuhakikisha mnapambana kwa kiwango cha juu kuitetea nchi yetu kwa kusaka matokeo chanya katika kila mchezo mtakaocheza kwenye fainali hizo. Mbali na kuonyes kiwango cha juu, ni wakati wa kudumisha nidhamu.

Inafahamika wazi hata kama mchezaji una kiwango cha juu, lakini nidhamu yao ni mbovu, unajiondoa mwenyewe kwenye nafasi ya kupata timu kutoka katika mataifa yaliyoendelea. Nidhamu ya ndani na nje ya uwanja ni muhimu kwa mchezaji.

Nipashe inawakumbusha wachezaji wa Stars kutumia michuano hiyo kama daraja la kusaka nafasi ya kwenda kucheza soka la kulipwa Ulaya na hiyo inawezekana kama mtaonyesha ubora na kuwavutia mawakala ambao wamefika Cameroon kusaka vipaji vipya.


Tunawakumbusha mashabiki soka na wadau wa michezo wote kuungana kuishabikia Taifa Stars ili ifanye vyema katika fainali hizo na hatimaye kurejea nyumbani na ubingwa wa michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

Kama ambavyo mashabiki wamekuwa wakizishangilia klabu zao hasa Simba na Yanga zinapokutana zenyewe kwa zenyewe au zinapokabiliwa na mechi za Ligi Kuu Bara au michuano ya kimataifa, huu ni wakati wa kutumia nguvu zaidi kwa Stars.

Nipashe inawakumbusha wake wenye uwezo wa kwenda Cameroon, wasafiri wakaishangilie Stars na wale ambao watashindwa, kuungana kwa pamoja kwenye kuiombea dua njema timu hii na hakika umoja wa mashabiki wa Simba na Yanga ukionekana kwa vitendo, Stars itavuna matokeo mazuri.

Mungu Ibariki Taifa Stars, Mungu Ibariki Tanzania. Pamoja tunaweza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hatuipendi Timu ya Taifa?

Na Barnabas Maro

**YASHANGAZA** kuwa wengi wetu hatuithamini timu yetu ya kandanda iitwayo Taifa Stars inayoiwakilisha Tanzania kwenye michezo ya kimataifa!

Zipambanazo Simba na Yanga jijini Dar es Salaam, Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao huingiza watazamaji 60,000 ilhali ule wa Uhuru huingiza mashabiki zaidi ya 20,000. Ni aibu iliyoje Timu yetu ya Taifa kushangiliwa na watazamaji 3,000 (kama wamezidi sana) kwenye viwanja vyenye uwezo wa kuingiza idadi kubwa ya watazamaji?

Ni aibu iliyoje kwa timu ngeni zinazokuja nchini kupambana na Taifa Stars kisha uwanja ukawa na watazamaji wachache sana wanaoishangilia timu ya nyumbani?

Hali hiyo huzipa nguvu timu ngeni kucheza kwa bidii na kushinda au kutoka sare ugenini na kutuacha tukiwalaumu walimu na wachezaji wetu! Watazamaji wanapokuwa wengi uwanjani na kuishangilia timu yetu, wachezaji hupata mori, yaani ari na hamasa ya kucheza kwa bidii zaidi.

Wengi wetu hatujui umuhimu wa kuishangilia Taifa Stars ila tunazishangilia Yanga na Simba kwa bidii na madaha/mbwembwe ilhali wengi wa wachezaji wa Taifa Stars wanatoka kwa vigogo hao wa soka nchini.

Utafiti niliofanya kwa watazamaji wachache wanaokwenda uwanjani kuishangilia Taifa Stars ni baadhi yao ndio wanaoharibu viti vya kukalia! Hukaa wakiwa wamekanyaga viti vya mbele visivyokuwa na watu!

Akili ni nywele kila mtu ana zake." Maana yake akili za watu hutofautiana kama zilivyo nywele kichwani. Methali hii hutumiwa kumzindua mtu anayeshangaa kuwa watu hufanya mambo kwa namna tofauti na afanyavyo yeye.

Pia "akili ya mtu ndio wazimu wake." Maana yake akili ya mtu yaweza kuwa wazimu wake pia. Methali hii hutumiwa kuelezea kuwa akili ya binadamu yaweza kuzua mema na mabaya vilevile.

Kero nyingine uwanjani ni wakati nyimbo za taifa zinapoimbwa kabla ya mchezo. Wachezaji wa timu ngeni pamoja na washangiliaji wao husimama kwa heshima huku wakiweka vitanga/viganja vya mikono yao vifuani na kufuatilia wimbo kwa maneno.

Wenzao wanapofanya hivyo kwa heshima, wachezaji wetu huwa tofauti wakati wimbo wa Taifa letu unapoimbwa. Labda ni mmoja au wawili tu ndio wanaofuatilia wimbo huo huku vitanga vyao vikiwa vifuani. Wengine husimama bila kuweka vitanga vyao vifuani wala kuimba! Ukiangalia upande wa watazamaji, wengine husimama kama waliolazimishwa, baadhi wakiweka mikono yao mifukoni, kuongea, kucheka na kupeana mikono! Hawajui umuhimu wa wimbo wa Taifa ambao unapoimbwa, watu hutakiwa kusimama ili kuonesha heshima.

Naomba nichukue muda mfupi kuhusu wachezaji wetu wa kandanda wanaostaafu kama alivyofanya Aggrey Morris majuzi. Mchezaji huyo wa Azam SC na Taifa Stars alisema anastaafu kwani vijana wanachipukia hivyo anaona ni muda sahihi kwake kuwaachia nafasi.

Kati ya zawadi alizopewa ni jezi ya Taifa Stars iliyosainiwa na wachezaji wa timu hiyo. Pia mfano wa hundi (hati inayoruhusu kuweka au kuchukua fedha kwenye akaunti benki) ya Sh. milioni tano.

Itapendeza kama vilabu vyetu vitakuwa na utaratibu wa kutoa zawadi zenye tija (faida) kwa wachezaji wao wanaostaafu. Kama ni wachezaji wa Taifa Stars, TFF nayo yapaswa kuwapa zawadi.

Wachezaji wa aina hiyo wanaweza kupewa viwanja au hata kujengewa nyumba. Vilevile wapatiwe mafunzo ya ualimu wa kandanda ili kuiwezesha Tanzania kuwa na walimu wananchi badala ya kuwategemea wa ughaibuni kama ilivyo sasa.

Wahenga walisema: "Mcheza kwao hutuzwa" wakimaanisha mtu anayecheza kwao hupewa zawadi au hutunzwa vizuri. Methali hii yaweza kutumiwa kutufunza kuwa mtu anayef anya jambo vizuri au inavyopasa, hutuzwa au hupewa zawadi.

Utaratibu huu waweza kufanya wachezaji vijana wajitume na kucheza kwa bidii wakijua mwishowe watatunzwa na vilabu vyao pamoja na TFF.

Natoa ushauri huu kwani baadhi ya wachezaji vijana hujitahidi ili wasajiliwe na Azam, Simba au Yanga ili watambulike nchini na nchi za nnje endapo timu hizo zitafanikiwa kucheza mechi za kimataifa.

Jumatano iliyopita, Yanga na Simba zilikutana kwenye fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa uwanja wa Karume mjini Zanzibar. Matokeo ni Yanga kuishinda Simba kwa kupigiana penalti baada ya dakika 90 kumalizika bila timu hizo kufungana.

# SIDA yafadhili wanafunzi 20 SUA

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA), imetoa ufadhili kwa wanafunzi 20 wa masomo ya Shahada ya tatu ya Uzamivu ya Sayansi za misitu wanaotoka nchi za Tanzania, Rwanda, Uganda, Msumbiji na Ethiopia kwenye Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Ufadhili huo unakusudia watakapohitimu masomo yao washiriki kikamilifu kusaidia kupunguza upotevu wa misitu inayoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi na kutatua changamoto zinazoikabiri misitu katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Akizungumza katika uzinduzi wa mpango huo kupitia programu ya Shahada ya tatu ya Uzamivu na kuwakaribisha, Mratibu wa mradi wa mafunzo wa Chuo hicho, Profesa Profesa Ishengoma, alisema umelenga kuokoa misitu ya ukanda inayozunguka nchi hizo.

Profesa Ishengoma, alisema mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden kwa kushirikiana na Shirika la Sida, unalengo la kupunguza upotevu wa misitu na kuendana na mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo kwa sasa imeikabili kwa kasi nchi za ukanda wa Afrika Mashariki.

Mratibu wa mradi huo, alisema wanafunzi hao watafanya utafiti unaojikita zaidi katika misitu ili kuona wanavyoweza kutatatua kero za misitu katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Alisema katika kipindi cha masomo yao darasani, wanafunzi hao watafundishwa na walimu kutoka kwenye vyuo vilivyo kwenye nchi zao ili kutengeneza programu moja.

Makamu wa Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Raphael Chibunda, alisema mradi huo chuoni hapo umedhihirisha ubora wa chuo hicho barani Afrika na duniani.

Alisema mradi huo umetokana na chuo hicho kuwa cha pekee katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika kinachofundisha, kumiliki misitu inayotumika kufundishia na kuzalisha mazao yatokanayo na misitu hiyo.

Kadhalika, alisema Chuo hicho kina eneo kubwa la misitu katika Mkoa wa Arusha-Olmotonyi, iliyopandwa katika Mkoa wa Tanga kwenye milima ya Usambaa eneo la Mazumbahi, ambayo ni wa asili wenye ukubwa wa ekari 320.

Alisema mwaka 2018, Chuo hicho kilipewa na serikali eneo la hekta 10,000 katika kijiji cha Ifinga, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, mkoani Ruvuma kwa ajili ya kuanzisha msitu wa mafunzo wa kibiashara, utafiti na ugani na tayari imepandwa miti hekta 800 katika eneo hilo.

# Aweso ataka mageuzi sekta maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewataka watendaji wote wa wizara kufanya mageuzi katika sekta ya maji ili kufanikisha lengo la kuwafikishia wananchi huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Waziri Aweso alisema hayo katika kikao kazi kilichowakutanisha watendaji wa wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake, kilichofanyika jijini Dodoma.

Alisema wizara imeajiri wataalamu wenye uwezo mkubwa wa kufanya mageuzi ambayo yatawezesha wananchi katika maeneo yote nchini kufikiwa na huduma ya majisafi na salama kwa wakati.

"Hatuwezi kuona wananchi wanakosa maji wakati sisi kama watendaji tupo, tunatakiwa kujitafakari kwa kina ili kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata majisafi, salama na yenye kutosheleza kwa wakati," alisema Aweso. Kadhalika, Aweso alisema umefika wakati kwa watendaji wa Wizara ya Maji kufanya kazi kwa bidii ili miradi ikamilike kwa wakati.

"Tusizoee kufanya kazi kwa mazoea na kujizoesha shida za wananchi kwa kukosa maji, kafanyeni kazi ili wananchi wapate majisafi na yenye kutosheleza na sisi viongozi wenu tupo nyuma yenu kuhakikisha azma ya serikali ya kuwafikishia wananchi majisafi, salama na yenye ubora kwa wakati," alisisitiza.

Waziri alisema mabadiliko ya bei za maji yaliyotakiwa kuanza kutumika kuanzia Januari, 2021 yasitishwe mpaka viongozi wa wizara watakapojiridhisha.

"Ni haki ya mwananchi kupatiwa huduma ya maji na ni wajibu wa mwananchi kulipa bili za maji na kushirikishwa wakati wa kusoma dira za maji ili kuondoa manung'uniko," alisema na kuongeza kuwa sio vizuri kuwabambikia wananchi bili za maji zisizokuwa na msingi.

Naye, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliwataka Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji nchini, Mameneja wa RUWASA, Mkoa na Wilaya kuwa na ushirikiano mzuri na viongozi wa serikali katika sehemu zao za kazi ili kuleta ufanisi katika kutekeleza miradi ya maji nchini na hatimaye kuwapatia wananchi majisafi na salama.




Mkuu wa Kitengo cha Fedha cha Tigopesa, Angelica Pesha (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 1.2 kwa Wakala wa Tigo Pesa mkoani Pwani, Angela Paschael, baada ya kuibuka mshindi katika hitimisho la promosheni ya Tigopesa Wakala Push, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanne wakiwamo raia wa Sri Lanka kortini madai kukutwa madini

**Na Hellen Mwango**

WATU wanne wakiwamo raia watatu wa Sri Lanka na Mtanzania mmoja wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kukutwa na madini mbalimbali yenye thamani ya Sh. milioni 45.

Washtakiwa hao ni Mohamed Hashim, Mohamed Muwas, Mohamed Yunus na Mehboob Rattansi (Mtanzania), wote kwa pamoja walisomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Godfrey Isaya.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa Januari 8, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa pamoja walitenda kosa la kuongoza genge la uhalifu kwa lengo la kujipatia faida.

Ilidaiwa kuwa, siku na tarehe ya tukio la kwanza washtakiwa hao walikamatwa wakimiliki gramu 2,054.4 za madini ghafi ya aina mbalimbali yakiwamo Rubi na Tanzanite yenye thamani ya Sh. 25,788,353.3 3 bila kuwa na kibali kutoka kwa Kamishna wa madini.

Ilidaiwa kwamba, Januari 8, 2021, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao kwa vitendo hivyo, waliisababishia serikali hasara ya Sh. 2,147,837.78.

Kosa jingine ni utakatishaji fedha, washtakiwa wote wanadaiwa kujihusisha katika miamala ya Sh. 42,921,055.49 wakati wakijua pesa hizo ni zao la kosa la kumiliki madini pasi kibali. Baada ya kusomewa mashtaka hayo, upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamlika na kuomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Januari 28, mwaka huu na washtakiwa warudishwe mahabusu kwa sababu shtaka la kutakatisha fedha halina dhamana.

# Chuo cha kijeshi kuanzisha hospitali utafiti magonjwa

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Kijeshi cha Sayansi na Tiba kimepanga kuanzisha hospitali yake kwa ajili ya kuimarisha utafiti, kuchunguza na kutibu magonjwa ya kuambukiza.

Chuo hicho ni chuo pekee cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kinachotoa mafunzo ya Stashahada ya Uuguzi na Stashahada ya Uofisa Tabibu nchini.

Hayo yalisemwa jana Lugalo, jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Chuo hicho, Brigedia Jenerali Charles Mwanziva, wakati akizungumza kwenye mahafali ya pili ya chuo hicho.

Wanafunzi 29 walihitimu Stashahada ya Uuguzi na wengine 20 Stashahada ya Ofisa Tabibu.

Brigedia Jenerali alisema kwa sasa wanategemea Hospitali ya Lugalo kwa ajili ya mafunzo ya vitendo na utafiti na kuanzishwa kwa hospitali ya chuo itakuwa hatua kubwa tangu kianzishwe mwaka 1972.

Vile vile, alisema wataalamu watakaohudumu kwenye hospitali hiyo mpya watatoka kwenye Hospitali ya Jeshi Lugalo na chuo kwa ajili ya kuimarisha maendeleo ya utafiti na mafunzo ya vitendo.

Alisema chuo pia kinatarajia kuanzisha maabara kubwa ya kisasa kwa kuwa hivi sasa wanategemea Hospitali ya Lugalo na pia wataanzisha maktaba ya chuo.

"Kwa sasa tuna uhusiano mzuri na vyuo vingine, lakini kwenye mpango mkakati wetu tunataka kuimarisha zaidi uhusiano huo ili tuweze kunufaika na utaalamu wa wenzetu ili chuo kiendelee kuimarika kwa sababu tunapata wanafunzi wa nje pia," alisema Brigeria Jenerali Mwanziva.

Alilishukuru Baraza la Ithibati Tanzania (NACTE) kwa kuwapatia miongozo mbalimbali na kuwapa ithibati iliyokisaidia chuo kupata uwezo wa kudahili wanafunzi wengi zaidi kutoka 500 tangu kuanzishwa kwakwe hadi kufikia zaidi ya 400 waliopo sasa.

Naye Mkufunzi Mkuu wa chuo hicho, Luteni Kanali Miraji Mawaka, alisema wanatarajia kuongeza kozi ya mamacheza (physiotherapy) na tiba ya meno ili kuongeza wigo wa udahili kwa wanafunzi wanaohitaji kusomea masomo ya afya nchini.

Luteni Kanali Mawaka alisema chuo hicho kilianzishwa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kupata wataalamu wa kuwahudumia askari wanapoumia vitani na kwenye makambi yao, lakini ikaonekana kuna uhitaji wa kupanua wigo.

"Tulianza kutoa mafunzo haya kwa maaskari, lakini baadaye tukapanua wigo kwa raia nao kujiunga na chuo hiki na hivi sasa ni kama nusu kwa nusu kuna wanafunzi ambao ni wanajeshi na wengine raia," alisema.



Wahitimu wa Stashahada ya Uuguzi na Uofisa Tabibu wa Chuo cha Kijeshi cha Sayansi na Tiba, wakiwa kwenye maandamano ya mahafali ya pili ya chuo hicho, yaliyofanyika Lugalo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Soko jipya kukusanya mil. 172/- kwa mwezi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro, inatarajia kuongeza mapato yake ya ndani kutoka Sh. milioni 48 kwa mwezi yaliyokuwa yakikusanywa kabla ya soko la zamani kuvunjwa na kufikia Sh. milioni 172.9 baada ya kukamilika kwa ujenzi wa soko kuu la kisasa.

Soko hilo la ghorofa moja limeanza kutumika Januari mosi, mwaka huu, baada ya kuvunjwa soko la zamani kwa sababu ya miundombinu yake kupitwa na wakati huku likichukua idadi ndogo ya wafanyabiashara.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Sheilla Lukuba, alisema hayo kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, wakati alipotembelea soko hilo ili kuona na kutatua kero zinazowakabili wafanyabiashara.

Lukuba, alisema miradi ya kimkakati iliyojengwa katika manispaa hiyo ukiwamo wa soko hilo, itaongeza mapato ya ndani na kuifanya manispaa hiyo kutekeleza majukumu yake kwa wananchi.

"Kwa kuwa hili soko ni jipya tumelifungua Januari mosi, mwaka huu, zipo kero zimejitokeza na sisi kama uongozi wa manispaa tutafanya tathmini ili kuwaondoa waliokiuka makubaliano kulingana na sheria za manispaa," alisema Lukuba. Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wafanyabiashara katika soko hilo walidai kuwa, vizimba vingi vimebaki wazi licha ya kuwapo wafanyabiashara wengi wanaovihitaji kwa ajili ya kuendesha biashara.

Walidai baadhi ya watu wasiokuwa wafanyabiashara wamehodhi vizimba na kuwapangishia wafanyabiashara halisi kizimba kimoja kati ya Sh. 50,000 na 70,000 kwa mwezi huku wao wakivilipia kwa bei halali iliyopangwa na manispaa ya Sh. 20,000 mwezi.

Soko kuu jipya la Morogoro, lina maduka 304, meza, 900 (vizimba), maeneo makubwa 16 ya kupangisha kwa mita za mraba kwa biashara kama benki, maduka makubwa, ofisi, migahawa, stoo tatu, vioski 34 vya mitumba na mabucha tatu zikiwamo sehemu za mama lishe.

Soko kuu la ghorofa moja limejengwa baada ya Wizara ya Fedha na Mipango kuipatia Manispaa ya Morogoro Sh. bilioni 17.6.

# Wananchi Keko walalamika tozo taka

**Na Maulid Mmbaga**

WAKAZI wa Keko Machungwa, jijini Dar es Salaam wamelalamikia tozo ya taka wanayotozwa na mkandarasi anayehusika na uzoaji katika eneo hilo kuwa kubwa na kutoendana na uchafu wanaozalisha.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Iddi Suleiman ameiambia Nipashe kuwa miaka mitatu iliyopita serikali ya mtaa ilifanya kikao na wananchi na kumtambulisha mkandarasi wa kuzoa taka na kutakiwa kulipa Sh. 3,000 kila kaya kwa mwezi.

Alisema kuna wakazi wengine hawazalishi taka zenye thamani hiyo na kuomba kiwekwe kiwango cha kulipwa kila nyumba badala ya kaya.

"Katika eneo letu kuna nyumba zingine zenye kaya zaidi ya 12, hivyo wanatoa Sh. 36,000 kwa mwezi, fedha hiyo ni kubwa na haiendani na taka tunazo zalisha na watu wanaohusika na kuzoa taka wanatoa risiti za mkono na wananchi hawajui pesa wanazo tozwa zinakwenda wapi," alisema Suleiman.

Alisema wananchi walipeleka malalamiko kwa Mwenyekiti wa serikali ya mtaa ya kuwataka wazoa taka kutoa risiti za kielektroni ili wajue kuwa kodi wanazozitoa zinaenda serikalini, lakini hawakupewa ushirikiano.

Alisema, hakuna mwananchi asiyetaka kuchangia kitu cha maendeleo, lakini wanahitaji kufahamu pesa wanayoitoa inakwenda wapi na baada ya kupeleka malalamiko kwa viongozi wao na kutofanyiwa kazi waliamua kugoma kulipa na baadhi walikamatwa na kuwekwa ndani.

Alidai kampuni hiyo inayohusika na uzoaji taka ilipochunguzwa iligundulika kuwa ni hewa na haitambuliki kisheria.

"Diwani alielezwa suala hilo, lakini hakutoa ushirikiano tukahisi labda kuna maslahi yake binafsi anayapata juu ya tozo hiyo kwani aliruhusu watu kukamatwa na kuwekwa ndani na alishindwa kuwapa mrejesho wananchi kuwa kampuni hiyo ilishinda tenda hiyo kiuhalali kwani imefanya kazi kwa miaka mitatu, lakini haina mashine ya kutolea risiti," alisema Suleiman.

Kuhusu suala la ulinzi shirikishi la kulipishwa pesa na wizi ukiendelea kwenye mitaa yao, alisema maeneo ya Keko vitendo vya uporaji vinaendelea watu wanaibiwa lakini wanaambiwa walipe Sh. 2,000 ya ulinzi na walinzi wapo saba ambao wanalinda watu zaidi ya 100,000 jambo walilodai kuzua sintofahamu.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Haji Omari, alipoulizwa kuhudu madai hayo, alisema malalamiko ya tozo ya taka aliyapata na wameshapeleka kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe na kuahidi kulishughulikia.

Alisema watu wanaofanya shughuli za uzoaji taka eneo hilo ni jukwaa la kinamama wa Migurani na walikopeshwa gari na risiti wanazozitoa zilizinduliwa na Mkuu wa wilaya aliyemaliza muda wake.

"Baada ya kupeleka malalamiko hayo kwa mkuu wa wilaya alieleza kuwa atakuja kutuletea mrejesho Januari 21, lakini kitu kinachosababisha jambo hili kuwa kubwa ni kikundi cha watu 10 wanaowahamasisha wananchi kugoma kulipa tozo hiyo hali inayosababisha gari la taka kushindwa kupita kwa kuwa watu hawalipii gharama za uendeshaji wa shughuli hiyo," alisema Omari.

Kuhusu ulinzi shirikishi, alisema kuna walinzi 15 na idadi kamili inayohitajika ni 20, lakini wananchi wa eneo hilo wanachangia kurudisha nyuma ulinzi huo kwa kuwa hawatoi ushirikiano kwa walinzi.

"Wananchi walipitisha wenyewe kuwa ulinzi shirikishi watachukua tozo ya Sh. 2,000 kwa kila kaya, lakini watu hawalipi na tulikubaliana kila mjumbe atoe vijana wawili watakaoshiriki katika ulinzi, lakini halikutekelezwa ipasavyo, wananchi wajitahidi kutimiza wajibu wao ili kumaliza changamoto zinazotukabili katika eneo letu," alisema Omari.



# Viwanda nchini kutengeneza simu janja

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WIZARA ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeanza mchakato wa kuanzisha viwanda ndani ya nchi ambavyo vitaanza kutengeneza simu janja.

Akizungumza juzi katika kikao kazi na Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi za Wizara hiyo, Waziri Dk. Faustine Ndugulile, alisema tayari utaratibu umeanza na kiwanda kimojawapo kinatarajiwa kujengwa Mwanza ili wananchi wamudu kununua simu hizo nchini.

"Ilani ya CCM inasema tupanue wigo wa mawasiliano na kuongeza matumizi ya intaneti, hatutaweza kufanikiwa kama wananchi hawatamudu kununua simu janja, na sisi tumeliona na ndani ya wizara tumeanza mchakato wa kuanzisha viwanda vyetu ndani ya nchi ambavyo vitaanza kutengeneza simu janja," alisema.

Alisema kiwanda hicho kitakachojengwa Mwanza kitakuwa kinazalisha simu hizo ambazo zitauzwa kwa Watanzania kwa bei nafuu.

"Nitoe rai kwa Watanzania mwekezaji yeyote mwenye nia ya kuwekeza kwenye Tehama aje kwenye wizara yetu na tutampa ushirikiano asilimia 100 kuhakikisha kwamba tunatengeneza bidhaa za Tehama ambazo zitatumika ndani ya nchi ili wananchi wapate simu janja kwa gharama nafuu," alisema. Alisema duniani pamoja na uwapo wa janga la corona kampuni zilizofanya vizuri na kupata faida kubwa zilikuwa za mitandao na kwamba Tanzania kwasasa inapiga hatua.

"Tuna vijana wabunifu, hakodi fremu kwa ajili ya biashara anaagiza biashara yake nje ya nchi, anafikisha nchini anaweka nyumbani anapiga picha na kutangaza mitandaoni na anauza kupitia mtandao na kukufikishia mzigo wako nyumbani, halipi kodi, hana leseni na hagombani na TRA," alisema. Alisema serikali itaendelea kutengeneza mazingira wezeshi na kuangalia jinsi ya kupata kodi kupitia biashara hiyo.

Alitoa wito wabunifu kubuni zaidi mitandao ambayo itasaidia nchi kutokana na mikubwa kuhatarisha na kutikisa baadhi ya nchi.

"Nimeona kuna mitandao mikubwa imeweza kumuathiri mmoja wa vigogo wa kubwa kwenye nchi moja duniani, sasa inaweza hata kuathiri nchi nyingine hivyo ni lazima na sisi kama nchi kuwa na mitandao ya kwetu ambayo itakuwa ya kitanzania yenye malengo yale yale na kupeleka nchi nyingine duniani," alisema.

Kadhalika, Dk. Ndugulile alisema wizara yake imejipanga kuboresha zaidi utoaji huduma kwa njia ya mtandao ili kurahisisha wananchi kupata huduma wanayoitaka popote alipo.

"Tunataka asilimia zaidi ya 70 ya huduma zinazotolewa na serikali zitolewe kwa Tehama ili kumpunguzia mwananchi bugudha ya kufuata huduma kwenye taasisi za serikali," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alimhakikishia waziri kuwa yote aliyoagiza katika kikao kazi hicho yatatekelezwa ili kufikia maono ya Rais John Magufuli ya kupanua wigo wa mawasiliano na matumizi ya intaneti.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (wa tatu kushoto), akiwa ameshikana mikono na viongozi wa kitaifa wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU), wakiimba wimbo wa mshikamano, wakati wa ufunguzi wa kikao cha Baraza Kuu la chama hicho Taifa, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mutungi avipa somo vyama vya siasa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MSAJILI wa Vyama vya Siasa nchini Tanzania, Jaji Francis Mutungi, amevitaka vyama vya siasa viendeleze siasa za kistaarabu na kuheshimu Katiba zao ili kukuza demokrasia nchini na kuondoa migogoro ndani ya vyama vyao.

Kupitia taarifa yake aliyoitoa kwa umma jana, Jaji Mutungi, alitoa wito kwa vyama hivyo kuendelea kutii Katiba na sheria za nchi.

Alitoa pongezi kwa vyama vyenye usajili wa kudumu kwa kuridhia kwao kushiriki uchaguzi kuu wa mwezi, Oktoba 2020 na kuzingatia suala la utulivu na utii wa sheria za nchi ikiwamo sheria zinazosimamiwa na Ofisi ya Msajili.

"Suala hili sio tu limedhihirisha ukomavu wa kisiasa bali limechangia mchakato mzima wa uchaguzi kumalizika kwa amani na utulivu.

"Ni matarajio ya mzalendo yeyote kuipenda na kuilinda nchi yake, ni kwa dhamira hiyo hiyo sisi kama wananchi wa Tanzania tunashukuru kwamba uchaguzi mkuu umemalizika salama na kwa amani na kuacha nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikisalia na umoja na mshikamano kama ilivyo desturi na utamaduni wetu," alisema.

Katika taarifa yake, Jaji Mutungi alisisitiza Watanzania kuendelea kuunga mkono maono ya Rais John Magufuli aliyoyatoa baada ya kuapishwa kwa kuwa uchaguzi sasa umekwisha badala yake wananchi wote bila kujali itikadi za vyama vyao wajikite katika harakati za kuleta maendeleo ya taifa na ustawi wa wananchi wake kwa ujumla.

"Ni kwa kuzingatia haya maono hayo aliyotoa Rais nimeona nitoe rai kuwaomba Watanzania hususan vyama vya siasa kwa umoja wetu, tuzingatie na kuyatekeleza kwa vitendo maono haya ya Rais," alisema.

Alivipongeza pia vyama vya CCM, ACT-Wazalendo na ADA TADEA kwa kuonyesha dhamira njema kisiasa na maendeleo kwa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar kwa maslahi ya Wanzanzibari.

"Huu ni ukomavu wa kisiasa waliouonyesha uwe endelevu na mfano wa kuigwa na vyama vyote vya siasa nchini bila kujali itikadi zao pindi linapojitokeza suala linalohusu utaifa na maendeleo ya nchi kwa ujumla," alisema.

# Mhagama ataka ripoti taasisi zisizounda mabaraza ya wafanyakazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Sera, Ajira, Vijana na wenye ulemavu, Jenista Mhagama, amemwagiza Msajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri nchini kuandaa ripoti ya Taasisi za umma pamoja na mashirika ambayo bado hayajaunda Mabaraza ya wafanyakazi.

Alitoa agizo hayo juzi jijini Dodoma, wakati alipokuwa akifungua kikao cha Baraza kuu Taifa, la Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU).

Alisema, taasisi nyingi za umma bado hazijaunda mabaraza ya wafanyakazi hali ambayo inawanyima wafanyakazi haki yao ya msingi kujadiliana mambo yanayohusu haki zao.

"Msajili nataka uniandalie ripoti haraka sana maeneo mengi bado hayana mabaraza ya wafanyakazi maeneo kama OSHA pamoja na TARURA bado hawana mabaraza haya kwanini hawana mpaka sasa inabidi niipate ripoti hiyo haraka," alisema Mhagama.

Alisema mabaraza yana umuhimu mkubwa kwa wafanyakazi kwa kuwa ni eneo linalowapa fursa ya kujadili haki zao na kero mbalimbali ambazo wanazipata kutoka kwa waajiri wao.

Pia, aliwataka wafanyakazi wote kuungana na serikali kupinga matumizi mabaya ya fedha za umma.

"TALGWU mnafanya vizuri sana katika kudhibiti matumizi mabaya ya fedha zenu, lakini hili mnatakiwa kulifundisha kwa wafanyakazi wetu kule wanakofanya kazi kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria na kanuni," alisema.

Vile vile, Mhagama alisema wafanyakazi wa serikali za mitaa ndiyo wamekuwa kwa asilimia kubwa wakikutana na wananchi wa hali ya chini katika utendaji wao wa kila siku, wanawajibu wa kuwa waadilifu katika maeneo yao.

"Kila siku wananchi wanakuta na maofisa watendaji wa vijiji, wauguzi, maofisa mifugo, maofisa kilomo hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia miiko ya utumishi wa umma na kutenda haki kwa Watanzania wanyonge," alisema Mhagama.

Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano kimataifa wa TALGWU, Shan Kibwasali, akisoma risala kwa niaba ya Katibu Mkuu Taifa, alisema kuwa moja ya matatizo wanayokumbana nayo ni watumishi wastaafu kutolipwa fedha za kurejea nyumbani baada ya kustaafu pamoja na kucheleweshewa mafao yao kwa mujibu wa sheria.

"Suala hili limekuwa ni kero hasa baada ya kuunganishwa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii, hivyo tunakuomba waziri utusaidie kuziagiza mamlaka husika kutatua suala hili ili watumishi walipwe mara baada tu ya kustaafu kwa mujibu wa sheria," alisema Kibwasali.





## CCM Z'bar yaomba Mahakama ya Mafisadi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, kimeiomba serikali kuanzisha Mahakama ya Mafisadi kama iliyokuwepo Tanzania bara ili kuona mali zilizochukuliwa zinarejeshwa ikiwemo fedha za wananchi.

Kimesema ni wakati sasa kwa Dk. Mwinyi, kuanzisha mahakama hiyo ambayo itatumika kwa watendaji wote wanaotuhumiwa na ubadhilifu wa mali za umma na ufisadi.

Katibu wa Kamati Maalum ya NEC Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Catherine Peter Nao, alitoa ombi hilo, wakati akizungumzia siku 71 za uongozi wa Dk. Hussein Mwinyi, tangu alipochaguliwa na wananchi kuiongoza Zanzibar.

Alisema kuanzishwa kwa mahakama hiyo kutaondoa usiri kwa waliokuwa wakijinufaisha wenyewe kwa maslahi yao na ufisadi utaisha kama inavyofanya Tanzania Bara.

Alisema kuwapo kwa chombo hicho kutasaidia kurudisha mali za wananchi na kuongeza heshima, ufanisi kwa watendaji wa taasisi za umma.

Alisema ufisadi ukiendelea kuachiliwa utaendelea kuiangamiza nchi na kuwa janga kwa Zanzibar, aliwaomba wananchi, vyama vya siasa na makundi mengine kumuunga mkono Rais wa Zanzibar, kushughulikia mafisadi ndani ya serikali.

Katibu Catherine alisema wapo baadhi ya watendaji hawakutekeleza wajibu wao ipasavyo katika serikali ya awamu ya saba na kumsaidia Rais mstaafu Dk. Ali Mohamed Shein, na kwamba wanapaswa kushughulikiwa katika mahakama hiyo.

"Katika uongozi wa Dk. Shein tukiri kwamba wapo viongozi wengine hawakuteleza wajibu wao na hawakumsaidia ipasavyo, kwani Rais Shein alikuwa kiongozi makini muwajibikaji na ndio maana ilani aliweza kuitekekeza kwa asilimia kubwa na ndipo Rais Mwinyi anaposema kila anapogusa kuna ufisadi," alisema.

Aliwasisitiza mawaziri waliopewa dhamana katika serikali ya awamu ya nane kuonyesha utiifu uliotukuka na kutofuata njia hizo ili kutorejea walipotoka.

Akizungumzia utendaji wa Dk. Mwinyi kwa siku hizo, alisema amekuwa muumini mkubwa wa kuondoa ufisadi, ubadhilifu wa mali za umma na rushwa katika serikali.

"Nitashangaa sana kuona mtu katika mitandao ya kijamii anatoa maneno ya kumkatisha tamaa au kumuona mbaya tuumunge mkono jambo hili, ili ufisadi uondoke kama ulivyoondoka Tanzania Bara," alisisitiza.

Alisema CCM inaridhika na hatua hiyo ambayo itaendelea kuleta heshima serikalini.

Alisema, Dk. Hussein Mwinyi anaendana na maneno na vitendo vyake kwa yale anayoyafanya juu ya dhamira ya dhati katika kuwatumikia wananchi na kusisitiza kwa methali ya 'Haja ya mna hunena Muungwana ni vitendo.

Alibainisha kuwa CCM imeridhika na utendaji wa Dk. Mwinyi ya ahadi zake katika kuwatumikia wananchi.

Vile vile, alisema tangu Dk. Mwinyi alipochaguliwa na wananchi wa Zanzibar amekuwa akionana na makundi mbalimbali hata katika nyumba za ibada ambazo wananchi wengi wapo na kusisitiza suala la amani.

Alisema ni dhahiri kuwa wananchi wa Zanzibar wamepata Rais mwenye kukubalika na kuona inasonga mbele kimaendeleo kwa haraka zaidi.

Alisema CCM inawaunga mkono viongozi wakuu wa serikali akiwamo Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kuonyesha uungwana na hatua yake ya kuungana katika serikali ya umoja wa kitaifa na kuwaomba wafuasi wake kumuunga mkono katika kuendesha serikali hiyo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (katikati), akiwafariji viongozi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kusini jana, kutokana na jengo la ofisi za chama hicho, kuungua kwa moto. **PICHA: OMPR-ZNZ**

# Wananchi waaswa kuwa watulivu jengo kuungua

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wanachama wa CCM na wananchi wa Wilaya ya Kusini Unguja kuendelea kuwa watulivu na wastahamilivu katika kipindi kifupi kufuatia jengo la ofisi yao ya chama wilaya kuungua moto.

Hemed Suleiman, alitoa kauli hiyo jana wakati alipozuru eneo la tukio hapo Makunduchi, kuona athari halisi na kuwapa pole wanachama hao pamoja na wananchi wa wilaya hiyo walioshirikiana kukabiliana na janga hilo.

Alisema Uongozi wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Serikali Kuu umepata faraja kubwa kutokana na nguvu kubwa ya umoja iliyotumiwa na wananchi hao ya kuuzima moto huo bila ya kujali Itikadi zao za kisiasa au kijinsia.

Makamu huyo ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, alisema hilo ni tukio linalomgusa kila mtu na kwamba nguvu za pamoja zitahitajika katika kuona jengo hilo linarejea katika uhalisia wa ubora wake na zaidi. Alisema vyombo vya dola katika kipindi hiki vinapaswa viachwe kufanya uchunguzi utakaobaini chanzo cha moto huo na kuviagiza viwasilishe taarifa kamili ya tukio hilo haraka iwezekanavyo ili kama kuna hatua zinazostahiki ziweze kuchukuliwa.

Abdulla aliwapongeza viongozi wa Mkoa Kusini Unguja kwa umahiri wao uliofanya CCM kuendelea kuwa imara ndani ya mkoa huo.

Alisema viongozi pamoja na wananchi wa mikoa mingine nchini wanaelewa kwamba Mkoa wa Kusini unabakia kuwa bora ikilinganishwa na mikoa mingine inayostahiki kufuata nyayo za mkoa huo.

Mapema Katibu wa CCM Wilaya ya Kusini, Hafidh Hassan Mkadam, alisema taarifa za ajali hiyo walizipata majira ya saa 12.20 jioni na kufika eneo la tukio muda huo huo.

Hafidh alimueleza Makamu wa Pili wa Rais kwamba harakati za kunusuru mali na vifaa ndani ya ofisi zilizoungganisha nguvu za wana-CCM na wananchi wa eneo hilo bila ya kujali Itikadi zao za kisiasa ziliwezesha kuokoa vifaa vichache ikiwamo mashine ya kudurusu.

Alisema kumbukumbu zote zilizokuwamo ndani ya ofisi hiyo vimeteketea na moto ambao hadi hivi sasa bado haijaeleweka chanzo chake.

# ZAWA yatakiwa kuongeza huduma ya maji

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati, Suleiman Masoud Makame ameitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), kuongeza huduma za maji katika maeneo mbalimbali ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa kulipa maji kupitia huduma ya Tigo pesa katika ukumbi wa ZURA, Maisara Mjini Unguja. Alisema kutokupatikana kwa huduma hiyo kikamilifu kutasababisha kutofikia lengo la serikali la kuongeza mapato kama sehemu ya kujiendesha kwa mamlaka hiyo.

Alisema kuimarika kwa mifumo ya ulipaji huduma za maji kutasaidia kuhamasisha wananchi kwa kiwango kikubwa, na kuwa mamlaka hiyo ina wajibu wa kuongeza vyanzo vya maji ili wananchi wafaidike na huduma hiyo.

Alizitaka taasisi za serikali na binafsi kulipia maji kwa wakati ili wananchi wapate huduma vizuri. "Awali wahudumu wa maji walikuwa wakipita nyumba hadi nyumba kukusanya ada hii jambo ambalo lilikuwa linawawia ugumu kuweza kuyafikia maeneo yote na kushindwa kupata makusanyo hayo kwa ufanisi," alisema.

Alisema hivi sasa dunia imeanza kutoka katika mfumo wa kizamani wa malipo na kuingia katika mfumo wa kisasa wa kidigitali. Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA, Mussa Ramadhan Haji, alisema wakati umefika kwa mamlaka hiyo kuhamia katika mfumo wa kielektroniki kupata makusanyo ya uhakika.

Alisema utekelezaji wa mpango huo ni kwenda na kasi ya awamu ya nane ili kuharakisha ulipaji wa huduma hizo na kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Alisema hivi sasa malengo yatafikiwa kwa kuona wateja wanapata huduma ya maji kikamilifu pamoja na kulipia kupitia mtandao huo.

"Tutahakikisha tunawahamisha wananchi kulipia huduma za maji, mamlaka hiyo itahakikisha kuwa inatumia mbinu za kisasa za elektroniki ya namna ya kulipia huduma za maji na tutatekeleza kwa vitendo kuanzia sasa," aliongeza.

Mkuu wa kitengo cha Tigopesa kutoka Tanzania Bara, Angelica Pesha, alisema lengo la kampuni hiyo ni kuhakikisha watu wanabadilika maisha na kuishi kidijitali kwa kutumia Tigopesa kupata huduma ikiwamo kulipa bili kirahisi.



POVU LA KUACHWA BAYA Ukurasa 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JANUARI 16, 2021





## KISICHORIZIKI HAKILIKI

# Esma, Msizwa cheko liko wapi?

FAIMILIA ya Diamond Platnumz, ipo katika njia panda kufuatia kinach-oendelea kati ya Esma na mume wake Msizwa, baada ya wawili hao kuonyeshana ubabe kila kukicha.

Wanandoa hao ambao wame-dumu miezi mitano tangu wafunge ndoa ya kifahari, kwa sasa wanatunishiana misuli na kuumbuana katika mitandao ya kijamii, kiasi ambacho kinaleta hofu.

Esma na Msizwa walifunga ndoa Juni mwaka huu 2020.

Katika ndo hiyo, Esma ambaye ni dada wa Diamond, aliolewa kuwa mke wa tatu ka-tika familia ya mfanyabiashara huyo mweye kazi yake Afrika Kusini.

Msizwa na Esma kwa sasa hapapikiki wala hapaliki, kila mmoja anaongea mabaya ya mwenzake na kibaya zaidi siri ya ndoa hiyo ikawekwa wazi na kuwaacha watu wakipigwa na butwaa.

Esma ambaye awali alikuwa kimya wakati Msiswa akilala-mika kusalitiwa na mke wake huyo, ameamua kuweka wazi kwamba yeye na mume wake hawakutarajia kuishi kwa muda mrefu kutokana na ndoa yao kuwa ya mkataba wa mwaka moja.

"Ilikuwa kama bahati kuishi kwa kipindi chote, ndoa yetu ilikuwa ya mkataba wa mwaka mmoja. Hatukukubaliana kuwa na mtoto, hivyo nilichoamua kupo wazi," amesema Esma.

Hata hivyo, Msizwa akizun-gumza kupitia redio ya Wasafi, amesikika akilalamika kuwa Esma amemfanyia tendo baya, ila anamuachua Mungu kwa kile alichokifanya katika maisha yake.

Aidha, katika posti yake moja Msizwa alimjibu shabiki yake mmoja kuwa hata bure hawezi kurudiana na Esma.

Kutokana na maneno makali wanayorushiana kupitia mitandao ya kijamii, baadhi ya watu wameshauri familia kutoka pande mbili kukaa ili kutuliza joto.

Hata hivyo, hakuna mwa-nafamilia hata mmoja aliye-jitokeza kuzungumzia sakata hilo, huku Msizwa akitupia la-wama familia ya Diamond ku-nyamaza kimya na kumuachia mtoto wao afanye kila anacho-taka kitu ambacho ni kinyume na maadili ya Kiafrika.

Uvumi kwamba wanandoa hao wametengana ilitokana na ukimya uliokuwepo kati yao jambo ambalo  watu kujiuliza maswali mengi ambayo ya-likosa majibu.

BASI SAWA

## Ben Pol kumbe una busara

MKALI wa miondoko ya R&B nchini, Ben Pol, amekwepa kuweka wazi siri ya yeye kubadili dini, akisema maisha yake binfasi yanabaki kuwa siri.

Akizungumza katika kipindi cha Friday Night Live, Ben Pol ambaye amebadili dini kutoka kuwa Mkristo na kuwa Muislamu, ameeleza suala la dini anawaachia wale anaokutana nao katika nyumba za kuabudu.

"Unajua wakati naanza muziki nilikuwa huru na mtu wa kila mtu ndio maana nataka iendelee kuwa hivyo masuala yangu binafsi kama dini sitaki sana kuyaongelea na hata picha zilivyotoka nikasema sitafafanua lolote ila tu kuna watu nitakutana nao kwenye nyumba ya kuabudu", amesema.



## 2021 yamwendea vizuri Ali Kiba

WAFUASI wa mwanamuziki, Ali Kiba, wamejikuta wakipagawa baada ya msanii huyo wiki hii kutambulisha ngoma tatu mpya zikiwa zote kali.

Alikiba ngoma yake ya mwisho 'MEDIOCRE' aliiachia mwezi wa tisa mwaka jana, lakini sasa ametambulisha ngoma tatu ambazo alishirikishwa.

Nyimbo hizo ni Nakupenza aliyoimba na DJ Sbu wa Afrika kusini, Proud Og You' akishirikiana na Darassa na In Love, ambayo ameimba na Otile Brown kutoka Kenya.





# Harmonize usishangae, kijana amekwishakua

MSANII nyota na bosi wa lebo ya Konde Gang, ameonyesha kushangazwa kwake na ngoma tatu za Ibraah ambazo amezitoa kwa pamoja.

Harmonize kupitia ukurasa wake wa Instagram, amehoji kama kweli Ibraah anajua maana ya maneno 'Karata tatu' ambayo yapo kwenye ngoma iitwayo Mapenzi.

"Mdogo angu Ibraah unajua uzito wa haya maneno? au umejiimbia tuu!!! daaaah dunia hiii sawa bana", - alisema sehemu ya ujumbe wake.



# Nai hivi ni kweli au maneno hayo?

MWANAMUZIKI mrembo wa Bongo Fleva, Nai ameapa kutofanya kazi na mpenzi wake wa zamani rapa Moni Centrozone.

Nai katika kusisitiza uamuzi wake huo, amesema yeye kwa sasa hana ukaribu na Moni na kuonekana kwake akiimba ngoma zake isichukuliwe anataka kurudi kwake.

Ameongeza kwamba muda uliopo anaangalia mipango ya kumuingizia pesa na hafikirii kuwa na mwanamume mwingine kwa sasa.



# Povu la kuachwa baya

**Na Adam Fungamwango**

KWA hali ya kawaida ya binadamu, kuachwa na mpenzi ni jambo baya sana ambalo hataki limtokee.

Mtu anapokuwa na mpenzi na wanapendana, anaona kama dunia yote ni ya kwake. Anatamani aote mabawa aruke juu na kuiambia dunia nzima jinsi gani anapendwa.

Hali inakuwa tofauti sana pale wanapoachana. Na hata mmoja anapoachwa. Unaweza kuomba ardhi ipasuke ili uingie.

Mtu anayeachwa anaweza kuona kama dunia yote inamuonea. Ataomboleza na kuongea yote. Wanamuziki na wasanii wanalijua hili. Ni watu anaoishi kwenye jamii na ama yamewakuta au wameyaona. Leo tuna nyimbo zinazowahusu watu walioachwa na wapenzi wao

**KUACHWA-KHALID CHOKORAA**

Wimbo huu ulitoka katikati ya miaka ya 2000, utunzi wake Khalid Chokoraa. Unazungumzia jinsi mtu aliyeachwa anavyojisikia vibaya. Mbaya zaidi ni kumuona mpenzi wake aliyeamuacha ananenepa, halafu yeye anakonda kwa mawazo. Ni moja kati ya vitu vibaya na usiombe yakukute.

**MAMA RHODA-JOSE CHAMELEONE**

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, msanii kutoka Uganda, Jose Chameleone, alitoka na wimbo unaosema 'Mama Rhoda'.

Mtunzi anamlalamikia mama Rhoda kwa nini amemuacha na anamwambia kuwa ipo siku atamkumbuka.

Ni kwamba mama Rhoda amemkimbia na kumuacha na watoto.

**SHAHADA YA UVUMILIVU-DDC MLIMANI PARK**

Ni wimbo wa masikitiko sana. Ulitungwa katikati ya mwishoni mwa miaka ya 1980. Ni stori ya mtu anayetunukiwa shahada ya uvumilivu na rafiki zake. Ni baada ya kukimbiwa na mkewe ambaye alirubuniwa na mwanaume kwa ahadi ya pesa na kujengewa nyumba. Jamaa ilimuuma sana, lakini hakulipiza kisasi cha hasidi aliyemrubuni mkewe. Badala yake aliacha kama ilivyo, lakini akiugulia maumivu moyoni.

**TUMA-JUWATA JAZZ BAND**

Katikati ya miaka ya 1980, Tx Moshi William alitunga wimbo wa 'Tuma', unaozungumzia mtu aliyesimama kwenye kona ya barabara za Uhuru na Msimbazi akiatazama wanaokwenda na kurudi kama anaweza kumuona mpenzi wake Tuma walioahidiana kupelekana kwa wazazi.

Jua liliwaka, hadi lilizama, demu hakuonekana. Jamaa alikuwa amechwa kwenye mataa.

Kwa huzuni, jamaa anaombolewa kuwa ni matatizo kumpenda mwanamke mrembo anayependwa na wengi, unaweza kunywa sumu au kujinyonga. Hata hivyo kwa kuwa yeye ni kijana, basi atasonga mbele na maisha mengine.

**MCHUMBA HANITAKI-SIMBA WANYIKA**

Ilikuwa ni mwishoni mwa miaka ya 1970, Willson Peter alipotunga wimbo wa 'Mchumba Hanitaki.'

Jamaa analalamika kuwa mchumba wake awali alikuwa anampenda na walipanga kuoana, lakini kwa sababu sasa pesa na kazi hana, ameamua kumsaliti na kumkataa mchana kweupe. Jamaa analalamika alie na nani.

# Ziwande; Ukiua kwa upanga, utakufa kwa upanga

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote bahati kama siyo yako, basi usiilazimishe. Tafuta nyingine au kitu kingine. Unapong'ang'ania kitu ambacho inaonekana kabisa kuwa hukupangiwa wewe, bahati si yako na badala yake unataka kung'ang'aniza ukipate kwa lazima au kwa hila, unaweza kufanikiwa kwa muda, lakini si kwa kudumu.

Filamu ya 'Ziwande' inazungumzia uroho wa mtu kwa kutaka kitu ambacho hakupaswa kukipata na badala yake anataka kukipata kwa nguvu.

Kutokana na kutumia nguvu, anasababisha madhara ya vifo kwa watu wasiohusika.

Kwenye kijiji fulani hapa nchini, aliishi msichana mzuri aitwaye Ziwande. Kila mmoja akawa anampenda.

Zuberi, mmoja wa wanakijiji wa hapo naye apia alimpenda Ziwande. Lakini Ziwande alikuwa hampendi. Lakini kutokana na uchawi alilazimisha apendwe. Penzi ni hiari, Ziwande alikuwa anakataa.

Mpwa wa Zuberi naye alikuwa anampenda Ziwande. Huyu kidogo ni kama msichana alielekea kumuelewa.

Zuberi alipogundua kuwa mpwa wake naye anamzengea msichana huyo anampiga mkwara wa hatari kuwa asirudie tena kufanya hivyo. Baadaye alijua nini lengo la mjomba wake. Kabla ya kufanya kitu chochote, Zuberi akamuua mpwa wake. Kisa tu ampate Ziwande.

Kuna kijana mmoja anaitwa Emma, alikuja kijijini kusalimia wazazi wake, akitokea mjini. Naye alipomuona Ziwande akampenda.

Ikabidi Zuberi sasa amfuate laivu Ziwande na kumwambia dhumuni lake la kutaka kumuoa. Ziwande akakataa katakata. Kwa hasira, Zuberi akaamua kumroga kwa kumpa kidonda ndugu.

Kisa tu kusiwe na mwanamume yoyote ambaye atakuja kumuoa. Nusu alifanikiwa. Ni kwamba Ziwande alikata tamaa ya maisha. Alikata tamaa ya kuolewa tena. Lakini pia hakuwa tayari hata chembe kuolewa na Zubari. Kijana Emma kutoka mjini alikuwa ameanza kufuata taratibu za posa.

Ugonjwa wa Ziwande haukumfanya kusitisha azma yake licha ya kwamba alitakiwa kutafuta mchumba mwingine hata na Ziwande mwenyewe.

Kila mmoja kijijini alimuogopa Zuberi kwa uchawi. Hakukuwa na wa kumfanya chochote. Emma alizunguka kwa waganga ambao wote walishindwa na nguvu za Zuberi.

Mwisho wa siku anakutana na mganga ambaye anampa kisu na kumwambia, iwapo Zuberi akikiona hicho, basi atamponyesha mchumba wake. Na hata akitoweka kimiujiza, basi Emma akichome chini, ataibuka tena.

Emma anafanya kama alivyoambiwa. Ujanja za Zuberi unakwisha. Anamponyesha Ziwande na yeye anauawa. Mwisho wa siku Emma na Ziwande wanaoana. Anayeua kwa upanga, hufa kwa upanga.





# Lady Gaga, Lopez kuimba Biden akiapishwa

WANAMUZIKI Lady Gaga na Jennifer Lopez, wataimba wakati wa sherehe ya kuapishwa Rais Mteule, Joe Biden itakayofanyika Ikulu ya Marekani.

Nyota hao walishiriki katika kampeni ya Biden wakati wa uchaguzi.

Lady gaga ambaye ataimba wimbo wa taifa hilo, alionekana katika mkesha wa siku ya uchaguzi wa mwezi Novemba mwaka jana na Lopez alimuunga mkono kikamilifu kiongozi huyo katika kipindi chote cha kuomba kura.





## Cindy shukuru wema wa Mungu

MSHIRIKI wa shindano la Big Brother Nigeria, Cindy Okafor, amenusurika kifo baada ya kupata ajali mbaya ya gari.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, mrembo huyo aliweka video fupi ambayo ilionyesha gari lake lilivyoharibika baada ya kutokea ajali hiyo.

"Nipo salama pamoja na watu ambao tulikuwa kwenye gari, Majeraha madogo tuliyopata lakini yote tunamshukuru Mungu kwa kutuokoa," amesema Cindy.

## Pole Victoria utapona

MWIGIZAJI wa filamu kutoka Nollywood, Victoria Inyama, amekutwa na maambukizi ya COVID-19 baada ya kupimwa mwishoni mwa wiki iliyopita.

Staa huyo kupitia ukurasa wake wa Instagram, ameweka video fupi ikimuonyesha akiwa hospitali akipatiwa matibabu.

"Nashukuru wote mnaoniombea, sikuwa mwangalifu wakati nawapeleka watoto shuleni, nimeambukizwa virusi vya corona," amesema.






## Shola uchungu wa mwana aujuaye...

SHOLA Ogudu, ambaye ni mama wa mtoto wa kiume wa mwanamuziki wa Nigeria, Wizkid, amemuwashia moto msichana mmoja baada ya kutumia picha ya utupu katika ukurasa wa Instagram ya mwanawe huyo.

Mama huyo alimkemea kwa kueleza mtoto wake Boluwatife, ana miaka tisa tu, sio jambo zuri kumtumia picha za aina hiyo.

"Mtoto wangu ana miaka 9 na kwamba hajafikia umri kupata vitu vya wazimu kutoka kwa msichana anayekua. Haiwezekani katika umri kama huo mnamtumia picha za ajabu," amesema.

## Naira Marley astaajabu ya mtoto huyu

STAA wa muziki kutoka Nigeria, Naira Marley, ameikubali video ya msichana mdogo akicheza wimbo wake.

Msichana huyo alionyesha kipaji chake cha kucheza wimbo wa mwimbaji huyo kwa ustadi wa hali ya juu.

Marley alimwuliza mama yake, kama kweli mtoto huyo hakuwa na baba.



MAKALA

# UGUNDUZI UNAOSHANGAZA

Na Mwandishi Wetu


Bonde la Olduvai limekuwa kiini cha utafiti wa chimbuko la binadamu duniani. **PICHA: MTANDAO**

## •Masalia ya zana za mawe yapatikana Tanzania
## •Zilitumika zaidi miaka milioni mbili iliyopita

Wanaikolojia wamegundua zana za mawe zilizotumika na binadamu wa kale miaka milioni mbili iliyopita.

Uvumbuzi huo umefanyika katika eneo la Bonde la Olduvai, Kaskazini mwa Tanzania.

Ugunduzi huo unatoa mwanga mpya kuhusu namna binadamu wanaoaminika kuwa ni wa kale zaidi walivyoishi na kumudu mazingira yao.

Ugunduzi huo pia unatoa jibu sahihi kuwa binadamu wa kale aliishi miaka milioni mbili iliyopita, na sio milioni 1.8 kama ilivyogundulika na watafiti wa awali.

Utafiti huo umechukua miaka mitatu na ulihusisha watafiti kutoka ndani na nje ya Tanzania.

"Tulianza utafiti mwaka 2017, ikatuvutia tukarudi mwaka 2018, tukitoka Olduvai tunarudi maabara, maabara tunakutana na changamoto, tukaendelea kutafiti, kwa sababu tulitaka tufanye kisayansi kabisa, tuliendelea hivyo ili tusiache mashaka hata kidogo kuhusu miaka laki mbili iliyoongezeka," alisema Dk. Pastory Bushozi, Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambaye alikuwa mmoja wa watafiti washiriki.

Watafiti hao wamegundua zana za mawe zipatazo 526 ambazo kwa mwonekano wake zinaonyesha uwepo wa zama mbalimbali za kuishi kwa mwanadamu.

"Katika kipindi hicho hicho tumegundua pia masalia ya wanyama tofauti wapatao 1,136 wakiwamo mamba, viboko na ndege na mabaki hayo yanaonesha kulikuwa na mazingira fulani ya uwepo wa mwanadamu," amesema Dk. Bushozi.

Nini kimesukuma utafiti huo kufanyika?

Watafiti hao wanasema waligundua uwepo wa viashiria vipya vya maisha ya mwanadamu katika eneo la Olduvai Gorge, ambalo linaaminika kisayansi kwamba mwanadamu wa kale zaidi aliishi hapo.

Awali walienda Kaskazini Mashariki mwa Bonde la Olduvai, chini ya miamba ambako masalia ya mwanadamu wa zamani yalipatikana, huko waligundua uwepo wa udongo ambao uliashiria jambo jipya.

"Tulitaka kujua huko chini ya miamba kuna nini? Tulibaini kwamba, kulikuwa na milipuko ya volkano ambayo ilifunika eneo hilo kabla ya hapo kulikuwa na maisha," alisema Bushozi.


Baadhi ya wataalamu wakichimbua masalia ya zana za mawe za kale.

Baada ya kutafiti zaidi, waligundua katika kipindi cha miaka laki mbili kati ya binadamu aliyeishi miaka milioni 1.8 iliyopita, ambaye anatambulika rasmi kama binadamu wa kale zaidi na mabaki waliyogundua hivi punde ya miaka milioni mbili iliyopita kulitokea na milipuko minne au mitano ya volkano.

Kubadilika kwa mazingira katika eneo hilo, kuliwafanya binadamu wa wakati huo kutengeneza zana mbalimbali ambazo ndizo zimeonekana sasa kwenye utafiti wao mpya.

Zipo zana za mawe ambazo, zinaonyesha uwepo wa zama tofauti za mwanadamu wa kale, lakini kwa muundo wake zinaonyesha kuwa zilikuwapo kabla ya miaka milioni mbili iliyopita.

Bushozi amesema kugundua kwa masalia hayo na zana za mawe ya kale, kumewafanya watafiti hao kubaini kwamba katika eneo hilo binadamu wa kale alikuwapo kwa zaidi ya miaka milioni mbili iliyopita.

Watafiti hao wanasema haikuwa kazi rahisi kutekeleza utafiti huo, kwa sababu ulileta maswali mengi kutokana na tafiti zingine za kisayansi za awali.

NINI KIMETOKEA?

Bonde la Oltupai kwa lugha ya Kingereza inajulikana kama Olduvai Gorge ni eneo la kiakolojia ni kati ya maeneo ya kale muhimu zaidi duniani. Bonde hilo linapakana na hifadhi mbili za wanayama ya Ngorongoro na Serengeti, ni mahali ambapo zamadamu, viumbe wa kale waliokaribiana. Waliishi tangu miaka milioni 2 hivi iliyopita, kwa mujibu wa utafiti wa sasa.

Eneo hili ni kivutio kikubwa cha cha watalii wengi wanaokuja nchini, ndipo chimbuko la mifupa ya wanyama kama tembo, kongoo wenye pembe kubwa na mbuni, mabaki ya fuvu la kichwa la Paranthropus boisei (pamoja na mumewe wa binadamu wa kwanza Zinjanthropus) ambalo lipo katika makumbusho ya Dar es Salaam, yaliyogundulika tarehe 17 Julai 1959 na mwanaakiolojia Mary Leakey.

Kwa mujibu wa watafiti hao, ugunduzi huo ni muhimu katika kuchochea utalii wa kiakiolojia nchini Tanzania.

**CHIMBUKO LA UTAFITI**

Miongo sita iliyopita, ugunduzi mkubwa ulifanyika katika eneo hilo la bonde la Oltupai, baada ya kugundua fuvu la mtu anayeaminika kuwa ni wa kale zaidi waliyompa jina la Zinjanthropus.

Ugunduzi huo uliofanyika saa nne asubuhi ya Julai 22, mwaka 1959, wakati huko kulikuwa na vipande zaidi ya 100 na ikasaidia kutambua asili ya watu wa kwanza duniani.

Kabla ya ugunduzi huo, wanasayansi na wanahistoria walikuwa wakiamini kuwa binadamu wa kale walitokea nchini China baada ya ugunduzi wa mafuvu ya kale kati ya miaka 1923 na 1927 inayofahamika kama Homo erectus, maarufu kama Peking Man. Mafuvu hayo ya China yalikuwa na umri wa takribani miaka 750,000.

Fuvu la binadamu la Olduvai lilikuwa na umri wa takribani miaka milioni 1.8, na hakuna mabaki ya mtu wa kale zaidi ambayo mpaka sasa yamegunduliwa.

Toka wakati huo wanasayansi na wanahistoria wanaamini kuwa asili ya mwanadamu ni bara la Afrika na eneo la Olduvai kwa yakini.

Lakini utafiti huu mpya unaleta majibu ya kwamba, binadamu wa kale, aliishi miaka milioni 2 iliyopita, ikiaminika kwamba, alitokea pia kwenye eneo hilo.

**NINI KINAFUATA?**

Pamoja na hatua hii mpya bado watafiti wanabaki na maswali kadhaa.

Katika eneo la Olduvai waligundulika aina mbili za zamadamu wa kale walioishi hapo, kuna Ancenstors ambao ni mababu zetu na Zinjis, lakini bado haijajulikana nani kati ya hao aliyetengeneza zana zilizogundulika hivi sasa.

Dk. Bushozi, anasema swali hilo linawafanya waone haja ya kuendelea kutafiti zaidi ili kupata majibu.

**BBC**

# Corona ilivyonyoosha nchi maskini kutegemea wafadhili

**Na Gaudensia Mngumi**



Baadhi ya makazi ya wanavijiji wa jimbo la Delta nchini Nigeria. Licha ya sehemu hiyo kuwa na mafuta mengi Afrika, wananchi ni fukara kupindukia. **PICHA:MTANDAO.**

MAZOEA ya mataifa maskini hasa ya Afrika kutegemea fedha za maendeleo kutoka kwa wahisani na mikopo ya benki za kigeni yameonyesha kuwa si endelevu na kuanzia sasa yatakuwa yamejifunza kutokana na kitisho cha COVID-19.

Tangu kuzuka kwa ugonjwa huo mapema mwaka jana imethibitika kuwa kuna haja ya mataifa hayo kubadilisha mikakati ya kutegemea wahisani kwa vile si endelevu.

Ni wazi kuwa kama Corona ingeendelea kutikisa bila kupata chanjo na 'lock down' au karantini, ni wazi kuwa ingefika siku Afrika ingekosa fedha za miradi ya maendeleo kama utaratibu waliozoea kuutumia usingebadilika.

Hilo linatokana na ukweli kuwa kumekuwapo na udhaifu katika kukusanya mapato na kutumia fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo badala yake, nchi zinategemea kukopa kwenye taasisi za kimataifa.

Mataifa mengi hukopa Benki ya Dunia (WB), ya Afrika, China, India na Falme za Kiarabu.

Inawezekana kwa mataifa mengi ya Afrika fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo hazikupatikana kwa wakati na pengine kiasi kilichopokelewa wakati huo wa corona pengine ni asilimia ndogo mno tangu kuzuka maradhi hayo mwanzoni mwa mwaka jana.

COVID-19 sasa iwe funzo kwa Afrika kuwa upatikanaji wa fedha za wahisani zama hizi ni kitendawili si kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, na huenda utaendelea kuwa wa kusuasua.

Fedha za maendeleo ni kama zinazohitajika kukarabati au kujenga barabara, reli, hospitali za rufani na kuziwekea vifaa tiba, vyumba vya madaktari na wodi na kuandaa wataalamu wakiwamo wa huduma za kibingwa.

Kama mataifa hayatabadilika na kuendelea kutegemea wahisani utafika wakati hospitali za Afrika zitakosa hata vitambaa vya gozi kwa ajili ya kusafisha vidonda, panadol za kutuliza maumivu na uchakavu wa majokofu ya kuhifadhi miili hautakwepeka.

Mwendelezo wa serikali kutunga bajeti zisizotekelezeka na zisizoleta mabadiliko zinazowangojea wakubwa kama WB, Benki za China, India na Umoja wa Ulaya zimepitwa na wakati.

Ni lini serikali zitatoka kwenye usingizi huo mzito wa kutegemea wafadhili?

**NIDHAMU YA MATUMIZI**

Suala la nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ni muhimu zama hizi na linahitaji kupewa kipaumbele cha kipekee. Kupambana na rushwa pamoja na usimamizi endelevu wa rasilimali za mataifa ni masuala yasiyokwepeka.

Afrika iache mazoea ya 'kuchukua chake mapema' na wizi wa fedha za umma. Watumishi wengi wa serikali hasa kwenye kusimamia fedha na mapato wako kwa ajili ya mkao wa kula fedha za maendeleo.

Kuanzia Afrika Kusini, Mashariki, Kati na Magharibi ubadhirifu ni jambo la kawaida, mikataba ya kiwekezaji ya kudhulumu wananchi, wizi wa rasilimali za Afrika ni habari za kila siku.

Viongozi wa bara hili wapate funzo kutokana na corona na kuachana na fikra za zamani kuwa watafanyaje kutumia fedha za umma kujinufaisha na familia zao.

Corona iwe funzo na kuachana na mazoea mabaya ya wizi, ubadhirifu na uporaji wa mali ya umma, watumishi wa umma na viongozi kuabudu ufisadi , hata yakijengwa madarasa, zahanati, barabara na huduma zinazotolewa hakuna viwango, kisa mazoea ya wizi, kila mmoja anachota, kisingizio mbuzi kula urefu wa kamba yake.

Iwapo Afrika itajitegemea itaona tija inayotokana na ufanisi wa kukusanya mapato. Pia, viongozi wake wawe na nidhamu ya matumizi kwa kupunguza ukubwa wa serikali zao na kubana matumizi. Waache kuunda wizara nyingi na kuwapa marafiki, jamaa na watoto wao vyeo na marupurupu yasiyonufaisha mataifa yao.

Ni wakati wa Afrika kuachana na kutoa misamaha ya kodi badala yake ikusanye mapato kutoka kwa wawekezaji na kuongeza vyanzo vya mapato.

Mara kadhaa umekuwa kama wimbo kuwa hakuna nchi iliyoendelea kwa kutegemea wafadhili wala wawekezaji wa kigeni, hili walione sasa.

Corona iwe funzo, hakuna nchi duniani iliyojengwa na watu kutoka taifa jingine, kwa mitaji na pesa kutoka ng'ambo.

Ni kwa sababu wawekezaji huondoka na mitaji yao, faida, rasilimali na teknolojoa na hawaachi kitu.

Tangu wawekezaji wageni waanze kuchimba dhahabu Congo, Ghana na almasi Tanzania wameacha kitu gani?

Wageni kwa miaka mingi walichimba mafuta kwenye jimbo la Delta nchini Nigeria, wakazi wa jimbo hilo wamepata maendeleo gani?shaba si maskini kuliko wote nchini humo.

Zambia inaongoza kwa uchimbaji wa shaba Afrika na hata duniani lakini wakazi wa Kitwe na Ndola yaliko madini hayo hawajabadilika.

Baada ya corona kila mmoja ashuhudie kuwa , kila mwanazuoni Dambisa Moyo, kutoka Zambia alichoandika kwenye kitabu chake cha 'Dead Aid' au 'misaada mfu' kinathibitika.

Ni ukweli kuwa hakuna lolote kwenye misaada, hivyo viongozi wa Afrika wafahamu kuwa ufadhili wa wahisani kwa kiasi kikubwa badala ya kuliwezesha bara kukua kiuchumi limedumaa na watu wake wameendelea kubaki maskini.

Moyo amethibitisha kuwa misaada hiyo ni kifo na kwa namna hiyo kuna kila sababu ya nchi za Afrika kuamka na kujitathimini kwa kuanza ukurasa mpya wa mikakati ya kujiletea maendeleo wenyewe, wakijifunza kutoka kwenye corona.

Ndiyo wakati wa kuachana na kununua samani 'duni' lakini ghali kutoka ng'ambo, kulipana mishahara, kusafiri ng'ambo kwa kutumia daraja la kwanza kwenye ndege, kuwa na misafara mikubwa kwenye ziara za viongozi ughaibuni na kulipana posho za fedha za kigeni.

Afrika isema hapana kwenye magari ghali na makubwa ya kifahari

Mabunge nayo yaache kuzorotesha maendeleo hasa kwenye uwekezaji na matumizi ya rasilimali yatunge sheria bora za uwekezaji na biashara za kimataifa, kadhalika yasimamie serikali ziwajibika kama ni ufisadi ziukemee na kuwawajibisha viongozi.

Afika imejaa sheria mbaya za uwekezaji hasa za madini, mafuta, gesi za kuruhusu wageni kuchimba na kuondoka na faida bila kuulizwa.

## Wavamizi Capital Hill walitaka kuwaua wabunge

**WASHINGTON,** Marekani

WAENDESHA mashtaka nchini Marekani, wamesema waandamanaji waliolivamia bunge wiki iliyopita, walikuwa na nia ya kuwateka na kuwaua wabunge.

Wakizungumza katika kesi moja ambayo inahusisha tukio hilo, walimtaka jaji mmoja aendelee kuwazuia Jacob Chansley kutoka Arizona na mtu mwingine aliyepigwa picha akiwa katika ofisi ya Makamu wa Rais Mike Pence, katika bunge la seneti wakati wa uvamizi huo.

Mawakili wa idara ya sheria kutoka Arizona, walielezea kwa kina kuhusiana na uchunguzi unaofanywa na idara ya upelelezi ya Marekani (FBI) kuhusu Chansley.

Chansley alitarajiwa kufikishwa mahakamani jana huku idara hiyo ikiwafungulia mashtaka zaidi ya watu 80 kuhusiana na uvamizi huo. **DW**

## Korea Kaskazini yaonyesha ubabe

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KOREA Kaskazini imefanya maonyesho ya makombora ya masafa marefu katika gwaride la kijeshi kusherehekea mwisho wa mkutano wa chama tawala nchini humo.

Katika maonyesho hayo yalioonyonyesha nguvu ya kijeshi ya nchi hiyo yaliyofanyika usiku wa kuamkia jana, yakiwa ya pili kufanyika katika kipindi cha miezi michache iliyopita. Kulingana na ripoti iliyopatikana, ilisema makombora hayo yalijumuisha yale yanayoweza kurushwa kutoka kwenye nyambizi.

Wataalamu walisema kuna uwezekano kwamba nchi hiyo ilikuwa inazindua aina mpya ya makombora yanayoweza kurushwa kutoka baharini pamoja na yale ya masafa mafupi. **DW**

## Zaidi ya watu 35 wafariki dunia

**JAKARTA,** Indonesia

WATU 35 wameuawa na wengine mamia kujeruhiwa baada ya tetemeko la ardhi lenye uzani wa 6.2 kuutikisa mkoa wa magharibi wa Sulawesi nchini Indonesia jana.

Tetemeko hilo limesababisha nyumba kadhaa kuanguka, huku idadi kubwa ya watu wakihofiwa wamefukiwa katika vifusi. Kulingana na mkuu wa shirika la kuwalinda raia, Darno Majid, wengi waliofariki walikuwa katika mji mkuu wa mkoa huo Mamuju.

Darno alisema juhudi za kuwanasua watu waliokwama kwenye vifusi bado zinaendelea.

Katibu wa gavana eneo hilo, Muhammad Idris, alisema hospitali mbili na jengo moja la ofisi za serikali ya mkoa huo pia zimeanguka. **DW**

UCHAGUZI UGANDA

# Museveni aongoza, Bobi Wine apinga matokeo

**KAMPALA,** Uganda

MATOKEO ya uchaguzi mkuu nchini Uganda, yameanza kutolewa huku Rais Yoweri Museveni anaongoza kwa kura nyingi.

Katika matokeo ya awali yaliyotolewa na Tume ya Uchaguzi jana asubuhi yalionyesha Museveni amepata kura 1,536,205 sawa na asilimia 65.02, mshindani wake mkuu Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, akipata kura 647,146 sawa na asilimia 27.39 kutoka vituo 8,310 vya kupigia kura.

Kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi, kuna jumla ya vituo 34, 684 vya kupigia kura nchini kote.

Hata hivyo, Bobi Wine amepinga matokeo hayo ambayo yanaelezwa ya kushangaza.

Bobi Wine alidai uchaguzi huo ulitawaliwa na wizi mkubwa wa kura ambao haujawahi kushuhudiwa katika historia ya Uganda.

**Wagombea walikuwa na mawakala ambao walishuhudia kuhesabiwa kwa kura katika vituo vya kukusanya na kuhesabu kura.**



Museveni



Kyagulanyi

Hata hivyo, mgombea huyo alitangaza kuwa mapambano ndio kwanza yameanza.

Awali wakati akizungumza na waandishi wa habari, alisema anaamini kuzimwa kwa mtandao kulivuruga uchaguzi huo.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Simon Byabakama, alisema kuwa Bobi Wine ana jukumu la kutoa ushahidi wa wizi na sio kutoa tuhuma.

Alisema wagombea walikuwa na mawakala ambao walishuhudia kuhesabiwa kwa kura katika vituo vya kukusanya na kuhesabu kura.

Ni vituo viwili tu vya upigaji kura vilivyoripoti kuwa na dosari na shughuli ya upigaji kura ilisitishwa.

Katika kituo kimoja mtu mmoja alitoroka na sanduku la kura. **BBC**



Baadhi ya wanajeshi wa Congo wakiwa msituni kuwasaka waasi wa ADF ambao wameongeza vitendo vya mauaji kwa raia. **PICHA: DW**

# Waasi wa ADF 46 waua DRC

**KINSHASA,** DR-Congo

WAASI wa kundi la ADF linaloendesha harakati zake mashariki mwa Congo, wamewaua watu 46 baada ya kushambulia kijiji cha Masini kilichopo katika Jimbo la Ituri.

Shambulizi hilo lilifanyika wakati watu hao jamii ya mbilikimo wakiwa katika makazi yao baada ya wanaume kwenda kuwinda msituni.

"Walijitokeza na silaha na kufyatua risasi, huku wengine wakiwaua watu hasa wanawake kwa kuwakata kwa mapanga. Na wanawake waliojaribu kutoroka, walipigwa risasi. Waliouawa ni wanawake pamoja na watoto." Alisema mkazi mmoja wa kijiji hicho.

Ripoti ya kuuawa kwa watu hao ilithibitishwa na mbunge wa kuchaguliwa wa wilaya ya Irumu, Jackson Aussen, ambaye alisema miili ya marehemu hao haijazikwa mpaka jana.

"ADF walishambulia kambi ya mbilikimo na kuwaua watu wote waliokuwamo kambini humo. Tukio ni baya kabisa." alisema Aussen.

Mashambulizi ya mara kwa mara ya waasi wa ADF katika vijiji mbalimbali vya wilaya ya Irumu mkoani Ituri, yamewavunja moyo wanaharakati wa haki za binadamu.

Christophe Munyanderu, ambaye ni mratibu wa shirika la kutetea haki za binadamu CRDH, aliiomba serikali kutilia maanani usalama wa raia katika Wilaya ya Irumu. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA VYUMBA VIWILI INAJITEGEMEA, PLOT NA 712/1,BLOCK 46

MAWASILIANO 0787233272
0674927560

## TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSTITUTE

INATANGAZA MUHULA MPYA WA MASOMO KOZI,KILIMO,MIFUGO NA MAENDELEO YA JAMII.CHUO KIMESAJILIWA NA NACTE REG.PWF/041/ KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI. 0752761280/0767574701 AU WWW.TRACDI.AC.TZ

## NAFASI YA KAZI

ANAHITAJIKA RIG BORING MACHINE OPERATOR 10' INCHES REVOVER
MAWASILIANO 0713 233334
0714 511696
DAR ES SALAAM

## KUPOTEA KWA VYETI



**ANDREW ANDREW MWAKANG'ATA** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,-cha kidato cha nne na transcript chenye index namba **S0341-0222** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **SANGU HIGH** mwaka 2014,cheti cha chuo **KILIMANJARO CHRISTIAN MEDICAL COLLEGE** kozi ya **PHYSIOTHERAPY** chenye index namba **NS0341/0222/2014** mwaka 2019,yeyote atakaevikota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa DAR/URA/RB/24369/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**YUSUPH JUMA MWENDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0445-109** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia MWEMBETOGWA SEKONDARI mwaka **1993.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: KJN/RB/4675/2019.**

## IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNALFOR MARA AT MUSOMA MISC. APPLICATION NO. 184 OF 2019

SHINJE MCHELE………………APPLICANT

VERSUS

1. JUMA JAKOBO MANYAMA
2. NYABUSU MCHELE
3. BUSANDA KASANDIKO……….RESPONDENTS

SUMMOUNS/NOTICE

TO
1. JUMA JAKOBO MANYAMA
2. BUSANDA KASANDIKO

The above mention applicant has instituted a suit at this court, against you, particulars of which are mentioned in a copy of application which is obtainable from the registry of this court,YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS COURT in persons(s) or by recognized agent(s) for mention on 20th January, 2021,2020 at 08:00 am in the fore noon

TAKE NOTICE THAT.

In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determine in your absence.

Given under my hand and seal of this Tribunal this 11 day of JANUARY, 2021.

Kitungulu, E
Chairman

The District land and Housing Tribunal- Mara

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Justinus Frederick Mafigi** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 684 DCT** Toyota - Corona Premio, **Eng: 3S7327023,** Chassis: **ST2100019969.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/RB/890033/2020

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW EMMANUEL SIMKOKO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 654 DCY TOYOTA CROWN ROYAL. CHASIS NUMBER GRS1830001664. ENGINE NUMBER 3GR55698.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: DAR/OST/RB/25347/2021.**




OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane - 4

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Mimi niko tayari kunyongwa ili nimfuate mpenzi wangu. Lakini nilishakwambia hata huko nyuma afande kuwa sitoweza kukubali kwa kinywa changu hiki kuwa nimemuua."

"Ndani ya gesti nzima hakukuwa na mtu yeyote zaidi ya wewe na mpenzi wako, sasa wewe unadhani ni nani atakuwa amemuua?"

"Hata mimi sielewi."

"Sasa nani ataelewa? Nani atakuamini?"

"Hakuna mtu yoyote duniani atakayeniamini, lakini ukweli ndiyo huo."

Inspekta Msiya hakutaka kujichosha na maswali ambao yalikuwa yakijibiwa hivyo hivyo kila anapomuuliza.

Akaamua kumpasulia ukweli sababu ya kumwita.

"Mimi nimekwita hata kukuambia kitu. Najua upo rumande hujui kinachoendelea. Ni kwamba kumbe mpenzi wako ni jambazi. Tena jambazi sugu." Aliacha kwanza angalie jinsi atakavyoipokea.

"Jambazi?"

"Ndiyo, wakati akija kwako na kuchukuana gesti, alikuwa ametoka kupora pesa, tena mamilioni. Inasekama alikuwa na wenzake watatu, wenzake wameuawa sehemu isiyojulikana na maiti yao kutupwa maeneo ya Kimara. Lakini yeye ndiyo amekutwa amekufa gesti na wewe ndiyo uliyomuua."

Mwanaidi alimwangalia kwa makini Inspekta Msiya, kilio chake kikakauka, akatabasamu.

"Mimi sikatai, inawezekana. Mimi ni mpenzi wake tu, sijui alikuwa anafanya kazi gani. Lakini afande nikuulize swali. Hivi kama Burhan alikuwa jambazi, hivi mimi kweli naweza kumuua jambazi?"

Inspekta Msiya alimtazama Mwanaidi, lakini hakumjibu kitu.

"Unaweza kutueleza ule mfuko wa pesa zaidi ya milioni 100 ulikwenda wapi?"

"Sijui. Hili swali nilishajibu afande, niliona mfuko, lakini mimi sikujua kama mlikuwa na pesa mle. Hii ya kusema kumbe Burhan alikuwa jambazi ndiyo unaniambia wewe, nilikuwa sijui."

************************

Wiki moja baadaye ilikuja barua kutoka kwa Mkuu wa Polisi. Ilimtaka Inspekta Kenneth Msiya aondoke Dar es Salaam kwa muda usiojulikana kwenye operesheni ya kusaka majangili kwenye hifadhi za mbuga za wanyama Katavi.




**Huoni kama ukipelekwa mahakamani kwa kesi hii adhabu yake ni kunyonywa hadi kufa au kifungo cha maisha kwa sababu ushahidi wa kimazingira unaonyesha kuwa wewe ndiye uliyetenda hilo kosa?**

Kwa maana hiyo, ilibidi akabidhi baadhi ya kazi zilizotakiwa kufanyiwa haraka kwa maafande wengine.

Moja ya kazi ambazo alikabidhi ni jalada ya upelelezi la mauji, linalomkabili Mwanaidi.

Hili alilikabidhi kwa mpelelezi Jan John. Alikuwa kijana wa miaka 30 tu. Kwa muda mfupi tu aliyojiunga na Jeshi la Polisi alikuwa amejipatia sifa kwa kuwa mjuzi wa kupata ushahidi wa kesi mbalimbali na kuharakisha kupeleka mahakamani.

Wakati mwingine, alisaidia mahabusu kuachiwa kutokana na uonevu au kugeuziwa kibao na baadhi ya watu wenye nia mbaya ya kulipiza visasi.

Alipendwa na wakuu wake wa kazi. Alipendwa na wafanyakazi wenzake. Alipendwa pia ni watuhumiwa na mahabusu pia, kutokana na kufanya kazi yake vizuri, bila kumpendelea au kumwonea mtu.

Afande Jan baada ya kupewa jadala hilo na mengine ambayo alitakiwa kuyafanyia kazi.

Siku ya leo aliamua kulifungia kazi jadala ya hilo la mauaji ya Mwanaidi dhidi ya mpenzi wake Burhan wakiwa gesti maeneo ya Kigogo.

Tayari alikuwa amemaliza kulisoma mara tatu. Baadhi ya vitu aliona vimekaa sawa. Vingine aliona vina utata na baadhi vilihitaji ufafanuzi.

Alimpigia simu Koplo Hamisi amlete Mwanaidi na yeye aanze kumhoji ili wamalize kukusanya ushahidi na kulipeleka mahakamani. Kama alivyoambiwa na Inspekta Msiya ni kwamba alifanyie haraka kwa sababu mtuhumiwa anakaribia mwezi mmoja sasa akiwa mahabusu ya polisi kwa sababu maalum tu.

Mbele yake aliletwa msichana. Macho yake yalimuona ni mrembo aliyechujuka. Angekuwa malkia kama angekuwa yupo huru nje, alioga vizuri, akivaa nguo anayoipenda, akisuka nywele kwa mtindo anaoutaka na kujipodoa kwa staili yoyote ile anayoiona inafaa.

Baada ya Koplo Hamisi kuondoka, afande Jan alibaki na mtuhumiwa Mwanaidi.

"Kumbe wewe ni mrembo hivi." Afande Jan alianza kwa maneno hayo. Ilikuwa moja kati ya mbinu zake mzuri za kumfanya mtuhumiwa awe huru na asiwe kama yuko kwenye hukumu.

Mwanaidi aliachia tabasamu, lakini lilikuwa na machungu ndani yake. Jan alitambua hilo.

"Jalada lako linasema kuwa unatuhumiwa kumuua mpenzi wako Burhan mkiwa kwenye nyumba ya wageni Kigogo. Halafu inadaiwa sababu ya kumuua ilikuwa ni kuchukua mfuko uliokuwa na pesa zaidi ya shilingi milioni mia moja ambazo mpenzi wako alizipora kwenye gari la kusambazia pesa kwenye vituo vya kuchukulia pesa ATM. Inasemekama baada ya tukio hilo mpenzi wako aliwaua wenzake na kwenda kuwatupa huko Kimara. Akaja na pesa hizo kwako," Afande Jan aliongea huku akiwa anatazama jalada badala ya kumtazama mtuhumiwa.

"Mkachukuana hadi gesti. Huko ukaziona hizo pesa. Ukamlagai kimapenzi, mlipomaliza akalala, ndipo alipochukua kisu na kumchoma nacho mara nne kifuani. Ukachukua mfuko wa pesa na kwenda kuuficha. Ukarejea kwenye eneo la tukio ukajilaza na kuzimia, lakini nia ilikuwa ni kujaribu kuwahadhaa polisi kuwa hukufanya wewe uhalifu huo, badala ya kukimbia ambapo polisi wangejua moja kwa moja kuwa muuaji ni wewe." Baada ya kumaliza kusoma aliinua kichwa na kumtazama binti huyo aliyeanza kutokwa na machozi.

"Kuna ukweli hapa? Mimi nimekwita hapa nikuulize tu maswali machache na si mengi, kwa sababu ulijibu kwa Inspekta Msiya na yapo hapa ameyaandika."

"Kuna mengine kweli, lakini mengine wananisingizia tu," aliongea kwa sauti ya kugugumia huku akifuta machozi kwa khanga aliyokuwa amevaa.

"Yapi ya kweli na yapi si ya kweli."

"Kwanza afande, mimi sijamuua Burhan. Lakini ni kweli alikuwa mpenzi wangu. Nilikwenda naye gesti na tukastarehe. Tulivyomaliza alinituma soda, niliporudi ndiyo nikakuta ameuawa."

"Alikuja na mfuko?"

"Ndiyo?"

"Baada ya kuuawa mfuko unaosadikiwa ulikuwa na pesa ulitoweka, ulikwenda wapi?"

"Waulize askari na watu waliokuja baadaye, mimi nilikuwa nimezimia, sikujua chochote kilichokuwa kinaendelea."

"Ulipotoka kwenda kununua soda nani alikuona?"

"Hakuna."

"Ndani ya gesti hiyo mchana huo kulikuwa na watu wengine."

"Sijui, lakini weita alihojiwa na polisi akasema hakukuwa na watu, ni mimi na Burhan tu."

"Weita hukumkuta wakati unakwenda kununua soda?"

"Sikumkuta?"

"Sasa tutaamini vipi kama kweli ulitumwa soda na kurudi ukakuta mpenzi wako ameuawa na siyo wewe ndiyo uliomuua?"

Mwajuma alibaki kanyamaza asijue la kujibu.

"Weita alikwenda wapi muda huo?"

"Sijui?" "Je, weita anaweza kuwa ndiye muuaji wa mpenzi wako na si wewe?"

"Hapo pia afande mimi siwezi kuelewa."

"Sasa wewe unachojua ni nini?"

"Afande, hakuna hata ninachojua, ingekuwa kama kitu cha kujiandaa, ningetafuta ushahidi wa kila njia ili kujinasua kwenye hili, lakini hakuna anayejua kesho itatokea nini, ndiyo maana kila kinachozungumzwa hapa mimi sijui chochote. Ninachojua ni mpenzi wangu Burhan ameuawa tu tukiwa gesti na mimi ndiyo naambiwa kuwa nimemuua."

"Huoni kama ukipelekwa mahakamani kwa kesi hii adhabu yake ni kunyonywa hadi kufa au kifungo cha maisha kwa sababu ushahidi wa kimazingira unaonyesha kuwa wewe ndiye uliyetenda hilo kosa?"

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# BARCELONA, MESSI WASHINDWA RUFANI




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeshindwa katika rufani yake juu ya kesi ya kadi ya njano aliyoonyeshwa Lionel Messi, baada ya kushangilia bao kwa kutoa heshima kwa gwiji, Diego Maradona.

Messi alitoa heshima ya kipekee kwenye mechi ya Ligi Kuu Hispania dhidi ya Osasuna baada ya kufunga bao, huku picha ya tukio hilo ikigonga vichwa vya habari baada ya mechi hiyo.

Katika kushangilia kwake, Messi alivua jezi yake ya juu, na kuonyesha jezi ya ndani yenye namba 10 kwa ajili ya kumwenzi Maradona.

Hata hivyo, baada ya mchezo kuendelea, mwamuzi, Mateu Lahoz alimpa kadi ya njano Messi na klabu ilitakiwa kulipa faini ya euro 3,000 kwa Shirikisho la Soka la Hispania.

Barcelona walikata rufaa juu ya uamuzi huo, lakini wameshindwa rufaa na Messi sasa atatakiwa kulipa faini ya euro 600 kwa mujibu wa kifungu cha 91 cha kanuni za nidhamu za Shirikisho la Soka Hispania.

Barcelona wana nafasi, na wanaweza kukata rufaa juu ya uamuzi huo kwenye Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo (CAS).

Japokuwa bado hakujaonekana dalili kama watachukua uamuzi huu, klabu inaweza kufanya hivyo ndani ya siku 15 tu baada ya kutolewa hukumu ya awali.

# Aubameyang: Kutofunga kunanitesa

**LONDON,** England

NAHODHA wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, amekiri amekuwa akihangaika sana msimu huu lakini ameamua kuufutilia mbali mwenendo mbaya pindi anapokuwa mbele ya lango.

Mshambuliaji huyo raia wa Gabon amefunga mabao matatu tu ya Ligi Kuu England msimu huu katika mechi 16 alizocheza hadi sasa.

Katika mchezo wa juzi Alhamisi usiku ambao Arsenal ilicheza dhidi ya Crystal Palace, pia Aubameyang hakuwa kwenye kiwango bora na hakuweza kucheka na nyavu katika mechi iliyomalizika kwa sare ya bila kufungana.


Kiwango kibaya cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 kilichangia kuanza msimu vibaya kwa washikabunduki hao wa jijini London.

"Kuanzia mwanzoni mwa msimu huu nilikuwa nikipambana sana, lakini nadhani hii ni sehemu ya mpira wa miguu," amesema Aubameyang akiambia Sky Sports.

"Tulijitoa kwa kiasi kikubwa sana mwishoni mwa msimu hadi kushinda Kombe la FA na kufuzu kwa Ligi ya Europa, kwa sababu ilikuwa muhimu sana kwa klabu.

"Wakati mwingine unakuwa na heka heka na lazima upambane kadri uwezavyo. Nilijaribu kadiri ya uwezo wangu na hadi sasa haikuwa nzuri sana kutoka kwangu.

"Mimi bado nina mtazamo chanya. ...dhani ninaweza kubadili jambo hii," ...ngeza kusema mchezaji huyo.






# *Hatima ya Rudiger Chelsea shakani*

**LONDON,** England

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Antonio Rudiger, ameripotiwa hawezi kuruhusiwa kuondoka Chelsea kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili endapo Fikayo Tomori ataondoka kwa mkopo.

Hatima ya Rudiger kuondoka kwa mkopo au jumla inategemea na klabu hiyo kama itamwondoa Tomori ambaye anatajwa kutakiwa kuondoka kwa mkopo.

Tayari klabu za Ujerumani na Italia zimetajwa kumhitaji Rudiger majira haya ya baridi.

Kwa sasa mchezaji huyo hana nafasi ya kudumu chini ya kikosi cha Chelsea kilichopo chini ya Kocha Mkuu, Frank Lampard, kwani Thiago Silva na Kourt Zouma ndio wanaopewa nafasi kubwa zaidi.

Kwa mujibu wa ripoti, Rudiger mwenyewe bado ana nia ya kutaka kuendelea kuichezea klabu hiyo ya jiji la London.

# Dembele atua rasmi Atletico Madrid

**LYON,** England

KLABU ya Lyon inayoshiriki Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, imethibitisha kuondoka kwa Moussa Dembele na kumkaribisha, Islam Slimani.

Dembele amejiunga na Atletico Madrid kwa mkopo huku akitazamia kusajiliwa kwa mkataba wa moja moja mwishoni mwa msimu huu.

Slimani ametua Lyon akitokea Leicester City kama mchezaji huru.

Atletico walihamishia nguvu zao kwa Dembele baada ya Napoli kukataa ofa ya timu hiyo kwa mshambuliaji, Arkadiusz Milik ambaye alitazamiwa kama mbadala wa Diego Costa.

Costa alikatisha mkataba wake na Atletico, na kocha, Diego Simeone akamtupia jicho Dembele kule Ufaransa.

Dembele anakwenda kuungana na Luis Suarez pamoja na Jao Felix katika safu ya ushambuliaji kwenye dimba la Wanda Metropilitano wakati ambapo Slimani ataungana na Memphis Depay katika kuhakikisha Lyon wanaendelea kuwachachafya PSG kwenye mbio za ubingwa msimu huu.



# MILAN YAKARIBIA KUMNASA MANDZUKIC




**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan imeripotiwa ipo kwenye mazungumzo na wakala wa aliyekuwa nyota wa Juventus, Mario Mandzukic.

Wakurugenzi wa Milan, Paulo Maldini na Frederic Massara ndio ambao wapo kwenye mazungumzo hayo ya kutaka kumsajili Mandzukic kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Kwa mujibu wa gazeti la Calciomercato, Mkurugenzi wa Ufundi, Maldini na Mkurugenzi wa Michezo, Massara wanafanya mazungumzo juu ya uwezekano wa dili la nyota huyu wa Croatia.

Taarifa zinasema Milan inataka kumpatia kocha Stefano Pioli uwanja mpana wa mbadala wa Zlatan Ibrahimovic, na mazungumzo tayari yanaashiria hatua kubwa ya kukamilika kwa mpango huo.

Taarifa nyepesi zinaainisha kuwa wakurugenzi hawa wanajaribu kukubaliana malipo na vipengele vya mkataba wa nyota huyu mwenye miaka 34.

Mandzukic aliachana na Juventus Januari mwaka jana, na akawa na mkataba wa miezi sita na Al-Duhail.

Nyota huyu tayari alishatumia miaka yake minne na nusu jijini Turin, akifanikiwa kufunga magoli 44 na kutoa pasi za mwisho 17 kwenye mechi 162 alizocheza na Juventus.

# *Nuno ataka kusepa Wolves*

**LONDON,** England

WAKALA Jorge Mendes anatajwa kuwa kwenye harakati za kutafuta timu nyingine kwenye Ligi Kuu England kwa ajili ya kocha, Nuno Espirito Santo.

Hii ni habari ya kushtua baada ya kocha huyo kusaini mkataba mpya na klabu ya Wolves hapo Septemba, mwaka jana.

Awali ilisemekana Mendes alikuwa na mazungumzo na Arsenal akimpigia upatu mteja wake (Nuno) akabidhiwe mikoba ya Mikel Arteta, tangu mambo yabadilike na Arsenal kuanza kupanda chati, maongezi ya kumpeleka mreno huyo Emirate yamekatishwa.

Kabla ya Ole Gunnar Solksjaer kukabidhiwa mikoba ya Jose Mourinho pale Manchester United, Mendes alipendekeza jina la Nuno, kabla ya viongozi kuamua kumchukua mtoto wao wa nyumbani (Ole).

Bado haijajulikana Nuno ataenda timu gani kama ataondoka Wolves, ingawa inasemekana timu atakayoenda lazima iwe inacheza mashindano ya Ulaya.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# WACHEZAJI ENGLAND 'NO' KUKUMBATIANA

**Serikali yatoa uamuzi huo kwa sababu idadi ya maambukizi ya virusi vya corona kuendelea...**

**LONDON,** England

BAADA ya idadi ya maambukizi ya virusi vya corona nchini England kuongezeka maradufu, serikali ya nchi hiyo imesema wachezaji na makocha katika michezo yote hawaruhusiwi kukumbatiana wala kupeana mikono, baada ya bao kufungwa na wakati wowote ule.

England imeshuhudia ongezeko kubwa la maambukizi ya corona huku zaidi ya watu 800,000 tayari wakiwa wamepoteza maisha katika nchi hiyo pekee kutokana na janga hilo ambalo tangu Machi 17, mwaka jana lilipoanza kusumbua duniani.

**Kwa mujibu wa BBC Sport, serikali imesema kuendelea kuwatazama wachezaji wakikumbatia wakati masharti kwa wananchi taifa hilo kuwataka kutofanya hivyo, kunaleta picha tofauti kwa hivyo ni heri sehemu zote masharti kuendana.**

Wakizungumza katika nyakati tofauti makocha wa Klabu za Ligi Kuu England, wameonekana kukubaliana na masharti hayo mapya ingawa wameonyesha utekelezaji unaweza kuwa na ugumu.

Makocha wa Manchester United, (Ole Gunnar Solskjaer), Manchester City (Pep Guardiola), na Newcastle United (Steve Bruce), kwa pamoja wamesema kwamba, pale bao linapatikana wachezaji wanaweza kujisahau.

Masharti ya kujikinga na maambukizi nchini England yamekuwa yakibadilika mara kadhaa, mwanzoni mwa Desemba, mwaka jana mashabiki walikuwa wanaruhusiwa kuingia baadhi ya viwanja kulingana na idadi ya maambukizi katika eneo hilo, lakini baadaye lilipigwa marufuku.

Bado haijulikana ni lini haswa hali hiyo itatengamaa huku baadhi ya mechi za ligi zikisitishwa pamoja na mashindano mengine.

## ZISIKUPITE

### RB: UPAMECANO HAUZWI

KLABU ya RB Leipzig haifikirii kumuuza mlinzi wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, Dayot Upamecano licha ya kwamba, anaweza kuondoka katika majira ya kipindi cha joto kwa dau la pauni milioni 37.4. Liverpool, Chelsea, Manchester United na Bayern Munich ni miongoni mwa timu zinazomnyatia. ***(Guardian)***

### IGHALO AITAKA MLS

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Odion Ighalo, mwenye umri wa miaka 31, anafikiria kuhamia katika Ligi Kuu Marekani, MLS. Uhamisho wake wa mkopo katika klabu ya Manchester United kutoka Shanghai ya China unakamilika mwisho wa mwezi huu. ***(ESPN)***

### SPURS KUMTEMA BALE

TOTTENHAM Hotspur huenda isiongeze mkataba wa mkopo wa mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31, kutoka Real Madrid kwa msimu wa 2021-22. ***(Times, subscription required)***

### LAMPTEY MAMBO SAFI

MLINZI wa Brighton, Tariq Lamptey mwenye umri wa miaka 21, anakaribia kuongeza mkataba wa muda mrefu na klabu hiyo ya Ligi Kuu England. Bayern Munich ni miongoni mwa klabu ambazo zinahusishwa na uhamisho wa beki huyo wa Timu ya Taifa ya vijana ya England chini ya umri wa miaka 21. ***(Talksport)***

### NEYMAR, PSG WATETA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 28, ameanza mazungumzo ya kuongeza mkataba katika klabu yake ya Paris-St Germain. ***(Sky Sports)***

### SPURS, CHELSEA VITANI

KLABU za Tottenham Hotspur na Chelsea zimeonysha nia ya kumsajili mlinzi wa kati wa Korea Kusini, mwenye umri wa miaka 24, Kim Min-jae, ambaye anachezea klabu ya Beijing Guoan ya nchini China. ***(Mirror)***

### DIA AINGIA SOKONI

WEST Ham inafikiria kumsajili mshambuliaji nyota wa Reims na Senegal, Boulaye Dia, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 akiripotiwa kwamba, anaweza kupatikana kwa dau la pauni milioni 15. ***(Eurosport)***

### VILLA YAMWINDA BROOKS

ASTON Villa ina nia ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Bournemouth na Wales, David Brooks, 23, katika dirisha hilo dogo la Januari. ***(Talksport)***

### GUILBERT AIGOMEA VILLA

MLINZI wa kulia wa Aston Villa na Ufaransa, Frederic Guilbert mwenye umri wa miaka 26, amekataa uhamisho wa kuelekea katika klabu ya Uturuki ya Istanbul Basaksehir. ***(Football Insider)***

### ARSENAL YAMTAKA SOLOMONI

ARSENAL ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia kwa karibu winga wa klabu ya Shakhtar Donetsk na Israel, Manor Solomon, 21, wakiwa na lengo la kuwasilisha ombi la kumsajili kipindi cha majira ya joto. ***(Guardian)***

HABARI MICHEZO

## Taifa Jang'ombe, Kilimani dimbani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Taifa Jang'ombe inatarajia kuendelea kusaka tiketi ya kurejea Ligi Kuu Zanzibar kwa kuwakaribisha Kilimani City katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Ligi hiyo inaendelea tena leo ikiwa ni siku tatu baada ya kumalizika kwa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, ambapo Yanga ya jijini Dar es Salaam iliibuka mabingwa wapya.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), ligi hiyo itaendelea katika mzunguko wake wa nne na leo kutakuwa na michezo mitatu tofauti.

Mechi nyingine zitakazochezwa leo zitakuwa ni kati ya Mchangani United dhidi ya New King ambayo itafanyika kwenye Uwanja wa Kinyasini Mkoa wa Kaskazini Unguja, huku Idumu ikiwavaa Mwembe Mkumbi City kwenye Uwanja wa Bungi uliopo Mkoa wa Kusini Unguja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa New King, Ame Dunia, alisema timu yake imejipanga vyema kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Dunia alisema Mchangani United ni moja ya timu ngumu lakini wachezaji wake watajitahidi kupambana na kutumia vyema uwanja wa nyumbani kwa mechi zote watakazocheza ili kujiweka katika mazingira mazuri.

## Majeruhi yamtesa nahodha Namungo

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Namungo FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Khamis Fakhi, amesema hali yake bado si nzuri kutokana na kusumbuliwa na majeraha ya mguu.

Fakhi aliliambia gazeti hili jana mguu bado unaendelea kumsumbua na kusababisha kushindwa kuitumikia timu yake hiyo yenye makao yake mkoani Lindi.

Nahodha huyo alisema anahitaji kupata ushirikiano kutoka kwa mashabiki wake katika kipindi hiki ambacho hali yake kiafya si njema.

"Mpaka sasa bado sijawa sawa, mguu unanisumbua, ninaomba mashabiki wazidi kuniombea dua ili nirudi uwanjani kama kawaida, naumia kuona nashindwa kuitumikia timu katika kipindi hiki muhimu," alisema Fakhi.

Aliongeza kwa kuushukuru uongozi wa klabu yake pamoja na wachezaji wenzake kwa ushirikiano wanaompatia tangu alipoumia.

Kuhusu mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambapo Namungo ilitolewa na Simba katika mechi ya hatua ya nusu fainali, nahodha huyo alisema michuano hiyo ilikuwa na ushindani na kila timu ilijipanga vizuri kuwania ubingwa huo uliochukuliwa na Yanga ya jijini Dar es Salaam.

# KOCHA MSIMBAZI ATAJWA KUOMBA KAZI GWAMBINA

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa Simba, Masoud Djuma raia wa Burundi anatajwa kuwindwa na klabu ya Gwambina FC ya jijini Mwanza ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

**Hata hivyo mabosi wa Gwambina FC bado wameshindwa kuweka wazi kuhusu mchakato wa kumwajiri kocha huyo katika timu yao.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Gwambina FC, Daniel Kilai, alisema klabu yake imepokea maombi kutoka kwa nchi tano tofauti akiwamo Mrundi huyo ambaye aliwahi kuifundisha Simba.

Kilai alisema makocha wengine walituma maombi wanatoka Italia, Ufaransa, Rwanda, Uganda, Kenya na Burundi kwa ajili ya kutaka kuchukua mikoba iliyoachwa na Fulgence Novatus ambaye walimwondoa.

"Kwa hapa nyumbani ni wengi sana, ni mapema kuwataja majina yao kwa ajili ya kulinda ajira za sasa kwa sababu wengi wao wapo katika mikataba na timu nyingine, kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Ufundi, Mwinyi Zahera tunaendelea na mchakato wa kupitia 'CV' hizo.

"Kwa sasa tupo katika hatua za kuhakikisha tunapata kocha sahihi na atakayeendana na vigezo vyetu, atakayetupeleka kufikia malengo yetu ya kucheza fainali ya mashindano ya Kombe la FA pamoja na kumaliza katika nafasi tano za juu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza wanatarajia kufunga mchakato wa usajili wa dirisha dogo kwa kuwapa mkataba wachezaji nyota watatu ambao ni pamoja na Mrisho Ngasa, Salim Aiyee na Mohammed Mussa kutoka Zanzibar.

Klabu hiyo iliamua kuachana na Novatus baada ya kupata matokeo yasiyoridhisha kwenye ligi hiyo ambayo tayari imeshaingia kwenye mzunguko wa lala salama. Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Gwambina yenye pointi 19, iko katika nafasi ya 14 baada ya kushinda mechi nne, sare michezo saba na imefungwa michezo sita.

Yanga ndio vinara wa ligi hiyo ikiwa na pointi 44 ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 35, lakini ikicheza mechi tatu pungufu.




Wachezaji wa Yanga kutoka kushoto ni Ramadhan Kabwili, Haruna Niyonzima na Mukoko Tonombe (kulia), wakiwa na kombe lao la ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwenye boti kabla ya kuanza safari ya kurejea jijini Dar es Salaam jana. Mwingine ni kocha wa makipa wa timu hiyo, Vladmir Niyonkuru. **PICHA: MTANDAO**

# *Coastal yafunga usajili na Mrundi*

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha la usajili likifungwa rasmi jana usiku, Coastal Union ilikamilisha mchakato huo kwa kumsajili kiungo mshambuliaji ambaye ni raia wa Burundi, Francis Mustapha akitokea Busarega FC ya nchini Rwanda.

Kwa nyakati tofauti, mchezaji huyo pia aliwahi kuzitumia klabu za Kiyovu Sports ya Rwanda na Gor Mahia ya Kenya.

Katibu Mkuu wa Coastal Union, Richard Mgweno, aliliambia gazeti hili Mustapha amesaini mkataba wa mwaka mmoja na ni baada ya kuridhishwa na kiwango chake.

Mgweno alisema Mustapha ni mchezaji wa sita kusajiliwa na Coastal Union kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo na uamuzi huo umetekelezwa ili kuziba mapengo ambayo yalitakiwa yafanyiwe kazi.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, alisema alikuwa anahitaji wachezaji wapya ili 'kuziba mapengo' aliyonayo, na sehemu ambazo aliziona zina matatizo ni idara ya ushambuliaji, ulinzi na kiungo mshambuliaji.

Mbali na Mrundi huyo, Coastal Union pia imemsajili kwa mkopo, Erick Msagati kutoka Polisi Tanzania, beki wa kati Mkongomani, Paul Kitenge kutoka As Nyuki na kiungo mshambuliaji wa Namungo FC, Jamal Issa Dulla.

Nyota wengine wapya waliotua Coastal Union ni beki wa zamani wa Yanga, Ally Ally akitokea KVZ na straika wa zamani wa Simba, Edward Christopher ambaye mara ya mwisho alikuwa akiichezea Kagera Sugar.

# Michezo



Jumamosi Januari 16, 2021

Nipashe

Hatima ya Rudiger Chelsea shakani UKURASA 20



Golikipa wa Yanga, Ramadhani Kabwili, akiwa amebeba kikombe cha ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi huku akizungukwa na mashabiki wa timu hiyo baada ya kurejea jijini Dar es Salaam wakitokea Zanzibar walikokuwa wanashiriki michuano hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga kujifua Arusha

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa mabingwa wa Kombe la Mapinduzi umesema unatarajia kukipeleka kikosi chao jijini Arusha kwa ajili ya kujiandaa na mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara itakayoendelea mapema mwezi ujao.

Kikosi cha Yanga kilirejea jijini Dar es Salaam jana mchana kikitokea Zanzibar, ambapo kilitwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi baada ya kuwafunga watani zao, Simba kwa penalti 4-3.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema wachezaji wa timu hiyo wamepewa mapumziko ya siku tatu baada ya hapo wataingia kambini kwa ajili ya kuendelea kujiimarisha kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu Bara na mashindano ya Kombe la FA.

Bumbuli alisema kambi hiyo ya Arusha itahusisha wachezaji wote waliobakia nchini pamoja na nyota wapya waliosajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo la usajili akiwamo Dickson Job.

"Kocha ametaka wachezaji wapumzike siku tatu, ila tutaangalia kama kuna uwezekano wa kuongezewa siku, lakini itajulikana baada ya Kaze (Cedric) kukutana na uongozi, kwa sababu ameomba timu iende kuweka kambi Arusha," alisema Bumbuli.

Naye Kocha Msaidizi wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema ubingwa walioupata ni ishara nzuri kwao kuelekea katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mwambusi alisema michuano ya Kombe la Mapinduzi imewasaidia kuboresha kikosi chao na kuwaongezea mbinu za kukabiliana na ushindani unaoongezeka katika kila mechi wanayocheza.

Yanga ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 44 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 35 lakini ikicheza mechi tatu pungufu.

# Ni Chikwende mali ya Simba

## ●●● Manara atamba kikosi chao sasa chazidi kuimarika na kutengeneza mfumo...

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI hatari wa FC Platinum ya Zimbabwe, Perfect Chikwende, anatajwa kuwa kwenye hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kujiunga na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam.

**Taarifa zilizopatikana jijini jana zinasema tayari Simba imeshafikia makubaliano na Chikwende ambaye aliwafunga katika mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa Mjini Harare Desemba, mwishoni mwaka jana.**

Hata hivyo, Simba bado haijamtambulisha rasmi mchezaji huyo, lakini Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Haji Manara, amesema ujio wake unakamilisha safu ya mbele imara itakayojulikana kama CCM akiwajumuisha na wachezaji wengine wawili, Clatous Chama na Luis Miquissone.

"Chama + Chikwende+ Miquissone= CCM. Ligi ya Mabingwa Afrika ndio yetu, kuchagua ni kupanga," alisema Manara.

Taarifa za Chikwende kutua nchini zilianza kutolewa na baadhi ya mitandao na magazeti ya Zimbabwe zikisema nyota huyo yuko nchini tangu juzi.

Gazeti la Newsday Sports la nchini humo lilimnukuu msemaji wa FC Platinum, Chido Chizolo, kuwa mchezaji huyo ambaye anaweza kucheza kama winga wa kulia na kushoto, aliondoka nchini humo Alhamisi na kuja jijini kwa ajili ya kujiunga mojawapo kati ya Simba na Azam FC, ambazo zilionyesha nia ya kuhitaji huduma yake.

Chizolo alisema tayari Simba ilikuwa imewasilisha ofa ya Dola za Marekani 55,000 kwa ajili ya kuvunja mkataba wake na klabu hiyo ambayo sasa itacheza mechi ya hatua ya mtoano katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Tunathibitisha hilo kuwa mchezaji huyo amekwenda nchini Tanzania, Simba wametuletea ofa na Azam nayo imeonyesha nia ya kutaka kumchukua pia," alisema mwanadada huyo akiliambia gazeti hilo.

Magazeti kadhaa nchini Zimbabwe yakinukuu vyanzo mbalimbali kutoka ndani ya klabu hiyo na baadhi ya wachezaji wa klabu hiyo ni kwamba mchezaji huyo aliyekuwa tishio kwenye mechi zote mbili za Ligi ya Mabingwa kati ya Simba dhidi ya FC Platinum, ameelekea nchini Tanzania kuwahi usajili wa dirisha dogo ambao ulifungwa rasmi jana usiku.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema klabu yake ilijiondoa kwenye mbio za kumwania winga huyo kutokana na kutokuwa kwenye mipango ya Kocha Mkuu, George Lwandamina.

Popat alisema Lwandamina aliwaambia anahitaji zaidi golikipa, na hivyo nafasi iliyobakia ya mchezaji wa kigeni ikajazwa na Mganda, Mathias Kigonya, kipa kutoka Forest Ranger ya Zambia.

Chikwende alifunga bao na kuwasumbua mabeki wa Simba katika mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa iliyochezwa nchini Zimbabwe na FC Platinum kushinda bao 1-0, kabla ya kugeuziwa kibao Januari 6, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kubugizwa magoli 4-0 na kutolewa kwenye michuano hiyo.

Pamoja na hayo, bado mchezaji huyo alionekana msumbufu, hivyo kuwavutia mabosi wa Simba na Azam FC waliofuatilia kiwango cha nyota huyo.

Simba ilifanya usajili kama huo kwa Miquissone ambaye baada ya kufunga bao nchini Tanzania akiwa na UD Songo ya Msumbiji, alisajiliwa na sasa ni mmoja wa wachezaji nyota kabisa kwenye kikosi cha Wekundu wa Msimbazi.

Chikwende anatajwa kuchukua nafasi ya mchezaji mmoja wa kigeni kati ya Benard Morrison ambaye ni mgonjwa au Francis Kahata anayetajwa huenda akatolewa kwa mkopo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >